



TPA kuwapa afueni ya tozo manusura K'koo Uk. 32

Rais Samia asimulia magumu aliyopitia

“Sina nia ya kujiingiza kwenye mjadala kuhusu suala hilo, lakini ninachotaka kusema ni kuwa baharia mzuri hujulikana wakati bahari ina dhoruba na siyo wakati bahari ikiwa shwari,” Rais Samia.



Habari Uk. 6

Simulizi kutoka ndani ya kifusi Kariakoo

Habari Uk. 14

RC Chalamila mikononi mwa Kamishna wa Maadili

Habari Uk. 40

Upelelezi utekaji Kiluvya ni ‘yaleyale’



David
Misime

SIKU 14 tangu Deogratius Tarimo, mkazi wa Kibaha, Pwani, anusurike kutekwa na watu waliotambulika sura zao, Polisi wanaeleza “yaleyale” kuhusu upelelezi wake.



Habari
Uk. 4

Tahariri/Katuni

Ujanja ni kupiga kura kupata viongozi

KESHO kutwa – Jumatano; Novemba 27, ni siku muhimu sana kwa Tanzania.

Ni siku ambayo kila Mtanzania mwenye sifa za kupiga kura atakuwa na fursa ya kufanya hivyo kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Katika uchaguzi huo, Watanzania watakuwa na nafasi ya kuchagua viongozi wao wa awali kabisa, ambao watawaongoza kwa kipindi kingine cha miaka mitano.

Jambo muhimu zaidi kwa Watanzania wenye sifa ya kupiga kura, ni kuhakikisha kwamba hawapotezi fursa hiyo adhimu ili kupata viongozi bora.

Tukumbuke kuwa kushiriki katika mchakato huu wa kupiga kura ni hatua ya msingi kuimarisha demokrasia na maendeleo ya taifa letu.

Kila kura inayoachwa ni sauti inayokosa nafasi ya kusikika, na kila mshiriki wa uchaguzi huu ana jukumu muhimu la kuhakikisha anasikika na kura yake inawapata viongozi wanawakilisha maslahi ya wananchi kwa uaminifu.

Zipo sababu zaidi ya 1000 za kuhimiza Watanzania kujitokeza kupiga kura, lakini Pambazuko linasema itoshe kuzitaja chache ambazo ni kujenga demokrasia imara.

Pia, kupiga kura ni haki ya kikatiba kwa kila mwenye sifa na njia bora ya kushiriki katika uamuzi unaohusu maisha ya watu ya kila siku na

maendeleo ya taifa.

Aidha, uchaguzi wa serikali za mitaa ni fursa ya kuchagua viongozi wa karibu zaidi ambao watahakikisha huduma za msingi kama maji, afya, elimu, na miundombinu zinaimarishwa - kama zipo na endapo hazipo, basi zinafuatiliwa ili zipatikane.

Pambazuko linaamini kuwa kwa kupiga kura, mwananchi anapaza sauti kwa viongozi na sera anazozikubali.

Kushindwa ama kukaidi kupiga kura, ni sawa na kuruhusu wengine wachague kwa niaba yako bila kuzingatia maoni yako, hivyo kuweka viongozi wasiokuwa chaguo lako.

Zaidi sana, idadi kubwa ya watu wanapojitokeza kupiga kura, kuna uwezekano mkubwa kabisa wa kupatikana kiongozi anayeaminika kushirikiana na wananchi kuimarisha amani na kuhimiza mshikamano wa eneo husika.

Pambazuko linawatakiwa Watanzania wote uchaguzi wa amani ambao utahakikisha wanapatikana viongozi bora wanaotarajiwa.

Kupiga kura siyo tu ni haki ya kila mwenye sifa za kufanya hivyo, bali pia ni wajibu wa kuchagua viongozi wenye maono na dhamira ya kweli ya kuboresha maisha ya wananchi.

Tukapige kura kuwapata watakaohakikisha Tanzania salama na yenye maendeleo.

Katuni



Mafunzo maalum...



Hivi karibuni Ofisi ya Ushirikiano wa Usalama ya Ubalozi wa Marekani, Dar es Salaam iliandaa tukio la kubadilishana maarifa na uzoefu kati ya wanajeshi wa Marekani na Tanzania kuhusu operesheni za masuala ya kiraia na huduma za kitabibu za kijeshi. Wanajeshi hutumika kwenye majanga wakati wa amani ili kuokoa uhai. (Picha na Ubalozi wa Marekani).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**

TIMU YA PAMBAZUKO

Mhariri Mkuu	:	Simon MKINA	(simon@pambazuko.or.tz)
Mhariri Mtendaji	:	Peter NYANJE	0784 211 716
Mhariri wa Habari	:	Maregesi PAUL	0689 732 325
Mwandishi Mkuu	:	Elizabeth HOMBO	0712 792 216
Mwandishi Mwandamizi	:	Andrew MSECHU	0769 415 815
Mkuu wa DTP	:	Yassin LUPATU	0782 009 971
Mkuu wa Utawala	:	Tryruckia MFINANGA	0744 768 263

Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A - nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz



Upelelezi utekaji Kiluvya ni ‘yaleyale’



Mkuu wa Jeshi la Polisi, Kamanda Camillius Wambura

Na Mwandishi WETU

SIKU 14 tangu Deogratius Tarimo, mkazi wa Kibaha, Pwani, anusurike kutekwa na watu walioambulika sura zao, Polisi wanaeleza “yaleyale” kuhusu upelelezi wake.

Jeshi la Polisi Tanzania ambalo limesaidiwa zaidi na kusambaa kwa video na habari ya Pambazuko, bado linaeleza “yaliyozoeleka” kwa umma juu ya matukio makubwa na mabaya – kwamba “upelelezi unaendelea.”

Novemba 11, mwaka huu ilithibitika pasinashaka kuwa watu watatu walioonekana sura zao walifika katika Hoteli ya Rovvenpec & Resort, iliyoko Kiluvya, Dar es Salaam, kwa ajili ya kuteka, lakini hawakufanikiwa.

Hadi leo, Jeshi la Polisi halijaweza kueleza umma endapo watuhumiwa wa tukio hilo wamepatikana au la.

Taarifa iliyotolewa na jeshi hilo mwishoni mwa wiki iliyopita ilieleza tu kuwa upelelezi bado unaendelea na upo katika hatua nzuri.

Juhudi za Pambazuko kuzungumza moja kwa moja na mmoja wa maofisa wa ngazi za juu wa jeshi hilo kutafuta hatua iliyofikiwa katika upelelezi wa suala hilo, ziligonga mwamba.

“Kumekuwepo na maswali na maoni mengi kutoka kwa waandishi wa habari na wana nchi wakitaka kufahamu hatua iliyofikiwa ya matukio mawili ambayo ni tukio la Deogratius

Tarimo, alilofanyiwa katika eneo la Kiluvya, Novemba 11, mwaka 2024 jijini Dar es Salaam na tukio linalohusu mmiliki wa jengo lililoanguka huko Kariakoo, Novemba 16, mwaka 2024.

“Upelelezi wa kesi hizi mbili, upo katika hatua nzuri na hivi karibuni taarifa kamili itatolewa kwa umma,” ilisema sehemu ya taarifa hiyo iliyosainiwa na msemaji wake, David Misime.

Kwa kuwa taarifa hiyo haikueleza jambo jipya kuhusiana na upelelezi huo, juzi Pambazuko lilichukua hatua ya kumtafuta Misime ili kujua iwapo watuhumiwa wa tukio hilo wame-shajulikana na kukamatwa.

Lakini Misime hakuwa tayari kuingia kwa undani kwenye suala hilo na kubaki na kauli inayofanana na taarifa aliyoitoa awali.

“Tumeshatoa taarifa, itumieni hiyo, sisi tunatoa taarifa ya kitaalam, hatuwezi kueleza kila kitu kilichoko ndani, umenielewa mzee,” alisema Misime na kucheka.

Tarimo, ambaye ni maarufu kwa jina la Deo Bonge, alinusurika kutekwa na kundi la watu watatu wiki mbili zilizopita katika hoteli hiyo maeneo ya Kiluvya.

Video ya tukio hilo, ikimuonyesha Tarimo akilalamika na kuomba msaada wakati akisukumizwa kwenye gari na watu hao, ilisambaa kwenye mitandao ya kijamii saa chache baada ya kurekodiwa na mtu ambaye alisaidia kuanika tukio hilo.

Katika video hiyo, Bonge anaonekana akiwa amedhibitiwa na wanaume watatu waliokuwa wakimvuta kwa nguvu kutoka hotelini hapo huku wakitaka kumuingiza kwenye gari lao ingawa walikwama.

Bonge alikuwa akiomba kusaidiwa ili watu hao, sura zao zilizoonekana dhahiri, wasimteke na kwenda “kumuua” – kama zilivyosikika kelele zake kuomba msaada.

Baada ya video hiyo kusambaa mitandaoni, Gazeti la Pambazuko lilifuatilia undani wake na kufanikiwa kutambua gari lililokuwa likitumiwa na watekaji hao. Lilikuwa na namba za usajili T 737 EGE aina ya Raum.

Rais Samia amenishangaza sana

Na Igo Al

KAWAIDA ya Mtanzania mmoja, mstaafu anayeishi kwa malipo ya pensheni, ni kuzungumza na wananchi kila wiki kupitia kwa waandishi wa habari.

Mwananchi huyo anayeitwa Mzee Tai, mkazi wa Mtaa wa Mpakani A, Kijitonyama, Dar es Salaam, wiki iliyopita hakupata wasaa wa kufanya hivyo kwa kuwa alikuwa kwenye maombolezo ya ndugu zake waliopoteza maisha baada ya kukandamizwa na wengine kukosa hewa kufuatia kuporomoka kwa jengo la biashara huko Kariakoo.

Mzee Tai hakutaka kusogelewa na kamera, vipaza sauti wala hakutamani kukutana na maswali ya waandishi wa habari, kwani aliamua kuuomba Mungu kwa kufunga – bila kula wala kunywa, kwa ajili ya kuwaombea ndugu hao.

Jana Mzee Tai ameita waandishi wa habari na kuwaleza kuwa amepokea kwa masikitiko makubwa maono ya Rais Samia Suluhu Hassan kwamba Tanzania na wananchi wake, siyo masikini.

Ameeleza kuwa amemsikia Rais Samia akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari vya Tanzania alioambatana nao huko Brazil kwenye mkutano wa matajiri wa dunia wa G20.

Mzee Tai akiwa ameivalia tisheti yake maarufu ya rangi ya kijani ikiwa na picha kubwa ya Rais Samia na kuandikwa – ‘Mitano Tena kwa Mama,’ amedai kusikitishwa na msimamo wa kiongozi huyo wa Tanzania kuhusu umasikini wa nchi na watu wake.

Amesema kauli ya Rais Samia kwamba umasikini unatafsiri tofauti kulingana na eneo kwake haibebi mashiko, kwani umasikini ni umasikini tu.

Mzee Tai anasema huenda Rais Samia amejielekeza vibaya kuhusu suala hilo la umasikini wa watu wake. Haiwezekani akaeleza kwamba hatambui kama watu wa “porini” wanaokula matunda na wanyama ni masikini.

“Mimi labda sijaelewa na hakika sipingani na

kiongozi wangu, lakini umasikini wa watu wa porini na maisha yao, yakilinganishwa na maisha mengine; haya ya kisasa umasikini wao unaonekana. Hakuna ubishi...”

“Lakini pia umasikini wa Watanzania, siyo lazima upimwe kwa watu wanaopenenda kuishi maisha yao; yawe ya kula matunda, kula mbogamboga, kukimbizana na kukamata digisigi na kuwala au yanayofanana...” “Umasikini wa Watanzania uko hata mijini, watu wanakula mlo mmoja, tena usiokuwa na ubora. Watu wanakosa baadhi ya dawa muhimu kwenye hospitali zetu. Watu wetu wengi hawana maji safi ya kunywa,” ameongeza Mzee Tai.

Lakini pia Mzee Tai akaongeza kwa kueleza kuwa visababishi vya umasikini wa Tanzania, Rais Samia anavijua, hivyo kikubwa anatakiwa kuvifanyia kazi na kuwaonya wanaoshikilia visababishi hivyo.

Tutumie tafsiri yako ushinde...



Huu ni mchoro wenye maana kubwa. Kila mmoja anaweza kuwa na tafsiri yake, hivyo gazeti la Pambazuko linatafuta tafsiri fupi, inayoelezeka na kufafanua vyema kuliko zote na itachapishwa na gazeti hili kwenye toleo linalofuata. Mhusika atatumiwa zawadi – Tuma tafsiri yako kwa simu: 0744 768 263.



Rais Samia asimulia magumu aliyopitia

Na Mwandishi WETU

RAIS Samia Suluhu Hassan amesimulia magumu aliyopita mara baada ya kuchukua kijiti cha uongozi wa Tanzania zaidi ya miaka mitatu ili-yopita.

Akizungumza jana baada ya kutunukiwa shahada ya heshima ya uongozi na Chuo Kikuu cha Mzumbe, Rais Samia amesema alipitia kipindi kigumu kwani kuingia kwake madarakani kuliambatana na matukio yaliyoiweka dunia katika hali ngumu kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Samia aliapishwa kuwa Rais wa Tanzania Machi 19, 2021 kufuatia kifo cha aliyekuwa rais wakati huo, John Magufuli.

Rais Samia alisema aliingia madarakani wakati dunia ikiwa inapambana na janga na Cpv-19.

Amesema katika kipindi hicho, dunia ilikuwa kama imefungwa na kusababisha biashara kusimama na hata watu hawakuweza kusafiri kwa uhuru kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine.

Rais Samia amesema katika mazingira kama hayo ilikuwa vigumu sana kutekeleza mipango ya serikali.

Amesema wakati hali hiyo ikiendelea, mara ikazuka vita kati ya Urusi na Ukraine, iliyosababisha kuyumba kwa uchumi wa dunia kwa kiasi kikubwa; kupandisha bei ya mafuta na gharama za usafirishaji.

Kiongozi huyo wa nchi amesema wakati 'akibangua' kichwa kufikiria jinsi ya kuendesha nchi chini ya majanga hayo, kukatokea mabadiliko ya sera za fedha nchini Marekani na kusababisha mawimbi makubwa kiuchumi duniani kote.

"Haya yalitokea wakati nchi tulikuwa tunatekeleza miradi mikubwa ya maendeleo ambayo ilikuwa inahitaji fedha nyingi," amesema.

Hata hivyo, Rais Samia aliiambia hadhira hiyo kuwa dhamira yake njema na sifa alizonazo kutokana na kulelewa vyema katika makuzi yake kiuongozi, vilimwezwesha kukabiliana na hayo yote na hivi sasa nchi inakwenda vizuri.

Rais Samia alibainisha kuwa zipo dhana mbalimbali kuhusu kiongozi, huku wengine wakisema kuwa viongozi huzaliwa hivyo wakati wengine wakisema viongozi hukuzwa.

"Sina nia ya kujiingiza kwenye mjadala kuhusu suala hilo, lakini ninachotaka kusema ni kuwa baharia mzuri hujulikana wakati bahari ina dhoruba na siyo wakati bahari ikiwa shwari," anasema Rais Samia.

Kwa mujibu wa Rais Samia mambo yaliyomwezesha kuhimili dhoruba na kufanikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wenzake katika uongozi, kufanya uamuzi akisukumwa na dhamira safi na kuweka mbele maslahi ya taifa katika kila alilolifanya akiwa kiongozi mkuu wa nchi.


Alibainisha kuwa suala la kujali maslahi ya taifa lilijidhihirisha wakati nchi zilipopewa fedha za mkopo wakati wa Covid-19 na kutakiwa kuzitumia fedha hizo kununua chanjo, barakoa pamoja na vitakasa mikono.

"Lakini tulipoangalia mahitaji yetu tukaona kabisa kuwa hayo hayakuwa mahitaji ya taifa letu kwa wakati ule..."

"Tukazitumia fedha hizo kujenga madarasa ya shule za msingi na sekondari, kujenga zahanati na kusambaza maji safi kwa sababu tulijua kuwa hayo ndiyo mambo yatakayotwezesha kukabiliana na janga la Covid-19 kama taifa," alisema.



Habarika kidijitali! Soma gazeti la **Pambazuko** na magazeti mengine maarufu kwenye **Rifaly!**



Scan to download Rifaly

www.rifaly.com



Uchaguzi Serikali za Mitaa



Ofisa wa Jeshi la Polisi akirekodi matukio kupitia simu yake ya mkononi mkutano wa Kiongozi Mstaafu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alipokuwa akiwaombea kura wagombea wa chama hicho katika Kijiji cha Nyankwi Kata ya Busunzu, Jimbo la Muhambwe mkoani Kigoma juzi. (Picha na ACT-Wazalendo)

ACT yapiga hatua kuunganisha upinzani

Na Mwandishi WETU

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimeonyesha wazi kwamba kiko tayari kwa ushirikiano na vyama vingine vya upinzani ili kudhoofisha Chama Cha Mapinduzi (CCM), Gazeti la Pambazuko limethibitisha.

Lakini hatua hiyo imekuwa kama mtego kwa vyama vingine vya upinzani kwani ni uamuzi ambao haukuvishirikisha.

Pia, ni uamuzi ambao umekuwa kwa kuchelewa sana – wakati kampeni za uchaguzi zimaeshaanza - kiasi kuwa imekuwa vigumu kwa vyama vingine navyo kutangaza kuungana mkono.

Hali hiyo imejidhihirisha wazi baada ya kamati ya uongozi ya chama hicho kutangaza hivi karibuni kuwaunga mkono wagombea wa upinzani katika maeneo ambayo hawakuweka wagombea katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajia kufanyika nchini kesho kutwa.

Chini ya utaratibu huo ambao siyo rasmi, wiki iliyopita viongozi wa chama hicho katika Mkoa wa Songwe, walimruhusu Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, asalimie wananchi katika eneo walilopanga kufanya mkutano wao wa kampeni katika Kijiji cha Mlowo.

Hata hivyo, Mbowe hakufanikiwa kuhutubia katika eneo hilo, baada ya Jeshi la Polisi Mkoa wa Songwe, kuwatawanya wananchi waliokuwa wamekusanyika mahali hapo kwa ajili ya kumsikiliza.

Taarifa hiyo ilitolewa juzi na Naibu Katiibu, Habari, Uenezi na Uhusiano kwa Umma wa ACT-Wazalendo, Shangwe Ayo, alipokuwa akizungumza na Pambazuko.

“Kamati ya Uongozi Taifa ya ACT-Wazalendo, imeagiza kuwa katika eneo ambalo mgombea wetu amekatwa, basi tunam-support (kumuunga mkono) mgombea wa upinzani na katika eneo ambalo hakuna kabisa mgombea wa upinzani, tunawahamasisha wananchi wapige kura ya hapana kwa mgombea wa CCM,” alisema Ayo.

Alipotakiwa kueleza kama vyama vingine vya upinzani navyo vinashiriki kuwanadi wagombea wa ACT-Wazalendo katika maeneo ambayo havina wagombea, Ayo alisema suala hilo linafanyika katika baadhi ya maeneo kwa kuwa lengo la wapinzani ni kukiondoa CCM madarakani.

“Hilo linafanyika katika maeneo mengi tu na mfano mzuri ni Njombe ambako Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake Chadema (Bawacha), Mkoa wa Njombe, Rose Mayemba, alishirikiana na wanachama wenzake wa Chadema, kumnadi mgombea wa ACT-Wazalendo.

“Huko Njombe ni mfano mzuri kisiasa kwani katika Kata ya Ruhuhu, Wilaya ya Ludewa, wapinzani kwa maana ya sisi ACT na Chadema, tumekuwa tukifanya kazi pamoja na umoja huo uliwasaidia kushinda vijiji na vitongoji.

“Yaani, hata kampeni zao kwa sasa wanazifanyia katika jukwaa moja, jambo ambalo ni zuri na linafaa kuigwa pia,” alisema Ayo.

Uchaguzi Serikali za Mitaa

CCM wakiwasha. Wasambaa kila kona



Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa ambaye pia ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dkt. Doto Biteko akisalimiana na wananchi waliojitokeza kumsikiliza katika mkutano wa kampeni za uchaguzi wa serikali za mitaa mkoani Geita jana. (Picha na CCM)

Na Mwandishi WETU

ZIKIWA zimesalia siku mbili kufika siku ya kupiga kura kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimesambaza kampeni zake kila kona ya Tanzania.

Chama hicho tawala hakitaki mchezo, kimedhamiria kupata ushindi mkubwa kwenye uchaguzi huu ili kudhihirisha ukuu wake.

Pamoja na kuwepo kwa tuhuma za kushirikiana na serikali ili kukihakikishia ushindi wake, CCM bado inang'ang'ana kwamba "inataka kushida kihalali."

Chama hicho kimesambaza viongozi wake wa kitaifa pamoja na makada mbalimbali katika mikoa yote nchini ambapo walishiriki uzinduzi wa kampeni na wanaendelea kuongoza kampeni katika maeneo yao hadi zitakapohitimishwa kesho.

Katika mgawanyo huo, Katibu Mkuu wa CCM, Dkt. Emmanuel Nchimbi, aliongoza kampeni za uzinduzi wa kampeni mkoani Mwanza wakati Naibu Katibu Mkuu wa CCM (Bara), John Mongela, alizindua kampeni hizo mkoa wa Mbeya, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Mohammed Said Mohammed, alipangwa mkoa wa Katavi na Katibu wa NEC, Organizesheni, Issa Haji Ussi, alipelekwa mkoa wa Geita.

Wengine walioshiriki kampeni hizo na mikoa yao kwenye mabano ni Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Amosi Makalla (Dar es Sa-

laam), Katibu wa NEC, Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUKI), Rabia Abdala Hamid (Kilimanjaro), Makamu wa Rais, Dkt. Phillip Mpango (Dodoma), Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (Kigoma), Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Abdulah Suleiman (Tanga) na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama hicho, Richard Kasesela (Songwe).

Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zuberi Ali Maulid (Singida), Mwenyekiti wa UWT, Mary Chatanda (Arusha), Waziri Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda (Mtwara).

Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama hicho, Halima Mamuya (Njombe), Mjumbe wa Kamati Kuu, Mohamed Aboud Mohamed (Iringa), Mjumbe wa Kamati Kuu, Jokate Mwehero (Pwani), Mwenyekiti wa UVCCM, Mohamed Ali Mohamed (Morogoro), Mjumbe wa Kamati Kuu, Nasir Ally Juma (Tabora) na Mwenyekiti wa Wazazi Taifa, Fadhi Maganya (Simiyu).

Wengine ni Naibu Waziri Mkuu, Doto Biteko (Mara), Mjumbe wa Halmashauri Kuu, Hussein Bashe (Shinyanga), Mjumbe wa Halmashauri Kuu Taifa, Salim Faraj Sabri (Ruvuma), Mjumbe wa Halmashauri Kuu Taifa, Ally Hapi (Kagera).

Wengine ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu Taifa, Livingstone Lusinde (Manyara), Mjumbe wa Halmashauri Kuu Taifa, Zainab Shomari (Lindi) na Mjumbe wa Halmashauri Kuu Taifa, Nape Nnauye yuko Mkoa wa Rukwa.

Mezani kwa Chahali

Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com



Vurugu za Msumbiji zaanika ujuha wa Afrika



Vurugu zinazoendelea nchini Msumbiji

HALI ya usalama nchini Msumbiji imekuwa ikikabiliwa na changamoto kubwa kutokana na vurugu baada ya uchaguzi zilizozuka kufuatia uchaguzi wa rais uliofanyika Oktoba 9, 2024.

Uchaguzi huu umesababisha mgawanyiko mkubwa wa kisiasa na maandamano makubwa ya umma, ambapo wapinzani walipinga matokeo yaliyotangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (CNE).

Matokeo ya tume hiyo yalionyesha chama tawala, Frelimo, kikiibuka na ushindi wa asilimia 70.67. Wakati huo, wapinzani walidai kuwepo kwa udanganyifu mkubwa katika mchakato wa uchaguzi.

Baada ya kutangazwa kwa matokeo, nchi ilishuhudia maandamano makubwa, hasa katika Mji Mkuu Maputo.

Hali hii ilizidi kuwa mbaya wakati polisi waliposhambulia waandamanaji kwa nguvu kubwa, ikiwemo matumizi ya risasi za moto na gesi ya kutoa machozi.

Ripoti zinaonyesha kuwa angalau watu 60 walikufa kutokana na ukatili wa polisi wakati wa maandamano haya.

Serikali iliamua kuzuia mitandao ya kijamii na kupunguza upatikanaji wa intaneti, hatua

ambayo ilionekana kama jaribio la kudhibiti habari na kuzuia maandamano zaidi.

Vurugu hizi zimeathiri vibaya uchumi wa nchi. Mipaka kadhaa imefungwa, ikiwemo ile kati ya Msumbiji na Afrika Kusini, hali ambayo imesababisha hasara kubwa kwa biashara na usafirishaji wa bidhaa.

Watu wengi wamepoteza maisha au kujeruhiwa, huku wengine wakikamatwa bila sababu za msingi. Hali hii inatia hofu kuhusu usalama wa raia na uwezo wa serikali kudhibiti ghasia.

Kwa sasa, serikali inaendelea kukabiliana na shinikizo kutoka kwa wapinzani na mashirika ya kimataifa kuhusiana na haki za binadamu.

Umoja wa Afrika (AU) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) wameelezea wasiwasi wao kuhusu hali hiyo na wamesisitiza umuhimu wa kufanya uchunguzi huru kuhusu mauaji yaliyotokea.

Wakati huohuo, viongozi wa upinzani wanasisitiza umuhimu wa kufanyika uchaguzi mpya ili kurejesha imani katika mfumo wa kisiasa nchini.

Katika muhtasari, hali ya usalama nchini Msumbiji ni tete sana kutokana na ghasia za baada ya uchaguzi zinazohusishwa na ukosefu wa uwazi katika mchakato wa uchaguzi.

Ni muhimu kwa serikali kuchukua hatua za haraka ili kurejesha amani na utulivu, pamoja na kuheshimu haki za raia katika kuandamana kwa amani.

Inashangaza zaidi kuona kuwa nchi nyingi za Afrika zinahofia maandamano hata kama haya na dalili za kutokea kwa fujo wala machafuko.

Hofu hii inafanya Afrika kuonekana kituko mbele ya uso wa dunia kwa kuwa inaharamisha hata haki za msingi za demokrasia.

Nchi nyingi zinaelezwa kuwa na katiba zinazoruhusu maandamano, lakini yanaonekana haramu kila yanapopangwa kufanyika.

https://instagram.com/evarist_chahali



Kuna maisha baada ya uchaguzi

VITABU Vitakatifu vinafundisha kwamba baada ya maisha haya ya duniani kuna uzima wa milele.

Jumapili ya mwisho kabla ya Majilio (Advent). Tumetafakari Kitau cha Luka 13:22-28.

Tukasikia habari za “Mlango mwembamba.” Tukatafakari jibu la mwenye nyumba: Nendeni siwajui enyi watenda dhuluma (Luka 13:28).

Kumbe katika Maandiko hayo kuna mengi ya kujifunza na kutambua ukuu wake.

Kwamba kumwamini na kumjua Yesu, sharti pia akujue.

Kwamba kula na hata kunywa naye siyo lazima akujue.

Kwamba Yeye kukufundisha njia zake siyo kigezo pekee cha wewe kuingia uzimani.

Kwamba kwenda kanisani, kuimba kwaya, kutoa sadaka na kutenda mengine yanayofanana na hayo au kuwa Myahudi mjukuu wa Ibrahim, Isaak na Yakobo tu - havitoshi.

Je, ni kwanini? Lazima kuna sababu ambazo zinamfanya Yeye asikufahamu.

Dhuluma Dhuluma Dhuluma. Hii ndiyo inakufanya umjue Yesu, lakini yeye asikujue. Ukibisha hodi anakuambia “Enenda zako, siku-jui wewe, mtenda dhuluma.”

Watu wafuatao wajihadhari zaidi kwani wanabeba machukizo mbele ya Muumba wao.

Wale wote wanaotenda hila, dhuluma, na kupotosha haki kwa kujua na kupanga kuwa wataomba msamaha baadaye kwa kigezo cha “Mwanzo Mpya,” “Maridhiano,” “Tugange yajayo” na tusameheane yaishe.

Wale wote wanaoona hila, dhuluma, na uovu wakakaa kimya kwa kudhani haiwahusu. Hawa ni wabaya kuliko watendao uovu na hawa wako daraja la kwanza.

Wale wote wanaowakatisha tamaa wanaopinga uovu, dhuluma na hila. Hawa ni waovu daraja la pili.

Wale wote wanaokubali kutumwa kufanya uovu wakidhani matokeo ya uovu watabeba waliowatuma. Hawa ni kuni za kuwachomea waovu daraja la kwanza na la pili.

Wale wote wanaopokea fedha ili wapishe uovu, hila na dhuluma vifanyike. Madhara na laana ya uovu huu huwa inaenda kwa vizazi vyao mpaka cha nne. Hata kwa kukanyaga mafuta, haiondoki.

Ni vyema binadamu tukakumbatia kutenda haki na kuenenda kwenye njia iliyoonyoka kwa kuepuka dhuluma na uonevu mwingine wote ambao ni chukizo kwa Mungu.

Sasa tunaanza wiki ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Kila mmoja akatende wema na kutimiza wajibu kwake kwa heri na kuacha dhuluma.

Kuna maisha baada ya uchaguzi. Kumbuke ni, kuiba kura ni uhaini. Ni sawa tu na ule wa kupindua serikali. Tuache dhambi hiyo.

Ileweke kuwa baada ya maisha haya, kuna uzima wa milele.

Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Jimbo la Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.





Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

Serikali itafakari upya mabasi kusafiri usiku

MWENENDO wa Serikali ya Tanzania umekuwa ni kusubiri kutokea kwa maafa ndipo hatua za kutafuta suluhisho zichukuliwe.

Utamaduni huu unaonekana kujirudia, ambapo badala ya kutangulia kwa sera madhubuti na hatua za kinga, nguvu huwekezwa kwenye hatua za dharura baada ya madhara kutokea.

Nikumbushe mifano michache ya tume zilizoundwa baada ya maafa zinaonesha udhaifu huu wa mfumo wa utawala unaozingatia matokeo badala ya kinga.

Nianze na Tume ya Uchunguzi Ajali ya mv Bukoba (1996); ajali ya meli iliyosababisha vifo vya zaidi ya watu 800 ilisababisha kuundwa kwa tume ya uchunguzi.

Tume ilibainisha ukosefu wa vifaa vya kisa vya uokoaji na uzembe wa mamlaka husika kwamba ni sababu kuu za ajali hiyo. Hata hivyo, mapendekezo mengi ya tume hayajatekelezwa kwa ukamilifu hadi sasa.


Kulikuwa na tume ya uchunguzi wa mafuriko ya Jangwani (2011); baada ya mafuriko makubwa yaliyoathiri eneo la Jangwani, Dar es Salaam tume ilichunguza athari za mipango mibovu ya matumizi ya ardhi na uchafuzi wa mito.

Hata hivyo, suluhisho la kudumu, kama kuhamisha wakazi wa mabondeni, halijafikiwa ipasavyo, na mafuriko yameendelea kutokea.

Wiki iliyopita tumesikia kumeundwa tena tume inayochunguza uimara wa maghorofa jijini Dar es Salaam kufuatia kuporomoka kwa ghorofa moja mitaa ya Kariakoo.

Ajali hiyo ilisababisha maafa makubwa baada ya jengo la ghorofa kuporomoka, na kusababisha vifo vya watu kadhaa na majeruhi.

Tume ya uchunguzi kama hii iliwahi kuundwa huko nyuma baada ya kuporomoka kwa jengo maeneo ya Chang'ombe, Dar es Salaam na



baada ya tukio hilo, tume iligundua matatizo ya ubovu wa ujenzi, udhaifu wa usimamizi wa mamlaka zinazotoa vibali vya ujenzi, na kutozingatiwa kwa kanuni za kiufundi.

Hata hivyo, hadi sasa, utekelezaji wa mapendekezo ya tume hiyo bado unategemea msukumo wa kisiasa na kijamii.

Baada ya mifano hiyo hapo juu, hoja yangu ni hizi safari za mabasi usiku zimekuwa zikisababisha ajali, lakini hakuna sera madhubuti za kudhibiti mwenendo huu.

Kwa mfano, ripoti zinaonesha kuwa madereva wengi wanaoendesha usiku hukosa usingizi wa kutosha, hali inayopunguza umakini wao.

Bila shaka hali hii inatarajiwa kuibua tume nyingine iwapo ajali mbaya itatokea, badala ya kuchukua hatua za kinga sasa kama kuisitiza safari za mchana pekee.

Kwamba mwenendo wa kusubiri maafa badala ya kuchukua hatua za kinga unapaswa kukomeshwa.

Serikali inapaswa kutumia vyombo vyake vya uchunguzi na kupanga mikakati ya kinga kabla ya athari kubwa kutokea.

Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com

Uchaguzi Serikali za Mitaa

Chadema hawataki mchezo. Hawajapoa



Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Nyasa, Joseph Mbilinyi akihutubia wananchi waliojitokeza kwenye mkutano wa kampeni za uchaguzi wa serikali za mitaa, Uyole mkoani Mbeya jana. (Picha na Chadema)

Na Mwandishi WETU

LICHA ya kuwepo kwa madai ya mikutano ya kampeni ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kuzingwa na serikali – kupitia Jeshi la Polisi, chama hicho hakijapoa. Kinachanja mbuga.

Chadema kimeapa kuendelea kufanya kampeni zake ili kuhakikisha kinapata ushindi kwa wagombea wake ambao wamepitishwa kugombea nafasi mbalimbali kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaofanyika kesho kutwa, Jumatano.

Katika kampeni zao, Chadema wamekuwa wakieleza sababu za kukiondoa chama tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM) madarakani kwa kuwa kimeshindwa kuwaletea nafuu ya maisha Watanzania.

Viongozi wa kitaifa na “makamanda” wengine wamesambaa maeneo mengi ambako kuna wagombea na kuendelea na kamoeni wakiamini kuwa watapata baadhi ya uongozi kwenye ngazi muhimu za awali za uongozi.

Viongozi hao wa chama hicho kikuu cha up-

inzani tangu kuanza kwa kampeni wamekutana na misukosuko, hasa kutoka vyombo vya ulinzi na usalama, na wamekuwa wakiilalamikia hali hiyo kuwa ina lengo la “kuwadhoofisha.”

Wanaamini kuwa purukushani hizo, zina mkono wa chama tawala, ili kisiweze kutimiza lengo kuu la kupata ushindi mkubwa kwenye uchaguzi wa mwaka huu.

Wakiongozwa na Mwenyekiti wa Chadema, viongozi hao wamesambaa nchi nzima ambako kila mmoja anafanya kampeni za kuwanadi wagombea wa chama chao.

Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, hadi sasa ameshafanya kampeni katika Kanda ya Nyasa inayohusisha Mikoa ya Iringa, Njombe Mbeya na Songwe.

Akiwa katika Mkoa wa Songwe, Mbowe alihutubia na kufanya kampeni katika maeneo mbalimbali yakiwamo Tunduma, Mlowo, Vwawa, Kyela, Rungwe, Mbeya Mjini pamoja na Mbeya Vijijini.

Aidha, Mbowe anatarajiwa kuhitimisha kampeni zake Kanda ya Kaskazini yenye Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara wakati Mbunge wa zamani wa Nyamagana, Ezekiel Wenje, yeye ameshafanya mikutano ya kampeni katika Mikoa ya Mwanza na Geita.

Makamu Mwenyekiti, Tundu Lissu, yeye alianzia Kanda ya Ziwa yenye mikoa ya Mwanza, Mara, Kagera na Shinyanga. Akiwa mkoa wa Mara, Lissu alifanya mikutano ya kampeni katika maeneo mbalimbali ikiwamo Tarime Mjini na Sirari.

Katibu mkuu wa chama hicho, John Mnyika, ameshafanya kampeni katika Kanda ya Kati kisha akaelekea Kanda ya Kusini yenye mikoa ya Mtwara na Lindi.

Naibu Katibu Mkuu (Zanzibar), Salum Mwalimu, amefanikiwa kufanya kampeni katika Kanda ya Serengeti kwa kuhutubia mikutano ya hadhara wilaya za Bunda na Kahama kisha akaelekea Kanda ya Magharibi na kufanya kampeni Mjini Tabora kabla hajaelekea Katavi, Mpanda, Tanganyika na Kavuu iliyoko mkoa wa Kigoma.

Na Dkt. Hellen Kijo
BISIMBA



Kona ya Dkt. Bisimba



Tusubiri tupate majanga kiasi kipi kujifunza?



Vikosi vya uokoaji vikiendelea na zoezi la utoaji kifusi kwenye eneo lililoporomoka jengo na kusababisha vifo na majeruhi hivi karibuni Kariakoo. (Picha na Mtandao)

TULIPOKEA kwa mshtuko taarifa za kuporomoka kwa jengo la ghorofa jijini Dar es Salaam katika eneo la Kariakoo Novemba 16 mwaka huu.

Kariakoo ni sehemu yenye watu wengi kutokana na kuwa na shughuli nyingi za kibiashara. Kwa kuwa ni kitovu cha biashara, eneo hili hukusanya watu kutoka maeneo yote nchini na hata kutoka nchi jirani.

Hii siyo mara ya kwanza kwa maafa kama hayo kutokea nchini.

Tumewahi kupata maafa makubwa ya kuzauma kwa meli ya mv Bukoba, Mei mwaka 1996 katika Ziwa Vitoria ambapo taarifa zinazonyesha kuwa walikufa zaidi ya watu 890.

Mwaka 2006 kuna jengo liliporomoka eneo la Chang'ombe, Dar es Salaam na kuua watu wanne. Wakati mwaka 2010 ilizama meli ya mv Spice Islander katika mkondo wa Nungwi na ilisemekana walikufa watu 203 na 619 kusalimika.

Novemba 2022 ndege ya abiria ya Kampuni ya Precision Air ilianguka ndani ya Ziwa Victo-

ria na watu kadhaa walifariki.

Haya ni baadhi tu ya maafa yaliyowahi kiumba nchi yetu. Kwa kuangalia tukio hili jipya la Kariakoo, yako mambo kadhaa ya kujihoji kuhusu utayari wa mamlaka za uokoaji yanapotokea matukio kama haya.

Mengi ya majanga haya yanaonyesha kukosekana kwa ufuatiliaji wa sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji wa mambo mbalimbali.

Tukianza na suala la uokoaji, tunaona katika matukio yote yaliyotajwa hapo juu kuanzia 1996 hadi 2022, kumekuwepo na hali ya wazi ya kukosekana utayari wa kuokoa, na hivyo watu kupoteza maisha au kujeruhiwa kwa vile tu huduma za uokozi zilichelewa au hazikufanyika kwa weledi wakutosha.

Baada ya jengo kuanguka Kariakoo kulikuwa na uzito wa kupatikana kwa vifaa sahihi vya kuokoa na ilichukua muda mrefu kiasi kwamba inaogopesha kuwa mamlaka zinazopaswa kufanya uokozi hazina vifaa vilivyopo tayari tayari kufanya uokozi mara tukio linapotokea.

Kuhusu jengo lililoporomoka Kariakoo, inaonekana kwa taarifa za awali kuwa kumekuwana ujenzi holela usiofuata taratibu.

Hii inashangaza sana kwani lilipoporomoka jengo kule Chang'ombe mwaka 2006, aliyekuwa waziri mkuu wakati huo, Edward Lowassa, aliunda tume iliyoangalia masuala ya ujenzi wa maghorofa katika jiji la Dar es Salaam na ilionyesha kuwa majengo 147 kati ya 505 yaliyokaguliwa hayakuwa na nyaraka na vibali sahihi vya ujenzi.

Tangu hapo, mambo inaelekea yalienda kama kawaida na wamiliki wa maeneo na majengo wakaendelea kufanya hivyo hivyo bila mamlaka husika kufuatilia ili kurekebisha kasoro hizo na kuchukua hatua ambazo zingeweza kunusuru hali kama iliyojitokeza Novemba 16 pale Kariakoo.

Nimeona viongozi wa serikali wakitoa mataamko na maelekezo lakini haya yanakuja baada ya mkasa na huenda baada ya vumbi kutulia, pasiwe na muendelezo.

Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.

Habari



Watembea kwa miguu wakipita karibu na kizuizi cha polisi kilichowekwa katika Barabara ya Msimbazi Kariakoo jijini Dar es Salaam jana ambayo imefungwa ili kupisha uokoaji na utoaji vifusi unaoendelea kwenye eneo lililoporomoka jengo na kusababisha vifo na majeruhi hivi karibuni. (Picha na Fidelis Felix)

Simulizi kutoka ndani ya kifusi Kariakoo

Na Arodia PETER

NI bahati ya mtende au ngekewa! Hivi ndivyo wanavyoamini vijana wawili ambao waliokolewa katika kifusi cha jengo la ghorofa tatu lililoporomoka Kariakoo na kuua watu.

Ajali hiyo ilitokea asubuhi ya Novemba 16 mwaka huu.

Walipokutana na Pambazuko ili kueleza mkasa huo, vijana hao; Amani Massawe na Hassan Yahaya, wanaanza kwa kumshukuru Mungu kwa muujiza wa aina yake aliowatendea hadi wakatoka salama kutoka katika lindi la giza, vumbi na mahangaiko ambayo hayakuonyesha matumaini makubwa ya kuwa hai.

Katika simulizi yao wanaeleza kuwa kusalimika kwao ni kama muujiza, kwani kuporomokewa na jengo lilikuwa ni tukio la ghafla ambalo halikuwapa hata chembe ya muda wa kujiandaa.

Ghafla walijishitukia wakiwa katika kiza totoro, huku hewa ikiwa imejaa vumbi, wasijue kilichotokea.

Lakini, baada ya muda, akili zilipowarudia baadhi yao, wakawasha tochi katika simu zao na hapo ndipo wakabaini kuwa wameangukiwa na jengo walimokuwa wakifanya biashara zao.

Hassan Yahaya, mkazi wa Mabibo Dar es Saaam, ni mfanyabiashara wa Kariakoo kwa miaka saba sasa akimiliki duka la suruali za kike

katika jengo hilo.

Yeye ni mmoja wa watu waliofunikwa na kifusi jengo lilipoanguka, lakini aliokolewa baada ya saa kadhaa.

Ingawa hakuwa chini ya kifusi kwa muda mrefu, lakini anasema mara baada ya tukio hilo akili yake ilimwonyesha kuwa mwisho wa maisha yake umefika. Aliamini kuwa si rahisi kuokoka katika hali kama ile.

Katika simulizi hiyo, Yahaya alisema, kabla ya jengo kuanguka na kuwafunika yeye na wenzake 26, alisikia kishindo kinachofanana na temeko.

“Kabla ya kutafakari tulikuwa tayari tumefunika, mle ndani lilikuwa giza tupu, hatukuwa na mawasiliano yoyote na watu wa nje kabla ya kuokolewa...”

“Tulikaa huko chini ya kifusi kwa wastani wa saa moja na nusu, kabla ya kuokolewa. Tukiwa kule chini na wenzangu, mawazo yangu yalikuwa nusu kwa nusu, yaani kifo na uhai...”

“Mle ndani eneo nililokuwepo mimi tulikuwa watu 26, na wote tuliokolewa na wakati tunatoka wenzetu katika maeneo mengine walikuwa bado hawajatoka...”

“Katika watu hao 26 tuliookolewa, wa kike walikuwa wanne na wengine waliobaki tulikwa wanaume...”

Inaendelea Uk. 15



Simulizi kutoka...

Inatoka Uk. 14

“Kule chini ya kifusi hakukuwa na mtandao wowote wa mawasiliano ya simu, unajua baadhi ya majengo ya Kariakoo ukiwa ndani hakuna mawasiliano, isipokwa huwa tunatumia kifaa maalum ambacho huwa kinavuta mawasiliano ya nje kuleta ndani...”

“Jengo lilivyoporomoka na umeme ulipokatika kifaa, hicho hakikuweza kufanya kazi, kwa maana huwezi kupiga simu wala kufanya chochote kwenye simu zaidi ya tochi...”

“Sisi ni kati ya watu waliookolewa mwanzoni walikuja watu kutuokoa na kutubeba kwa gari maalum ya wagonjwa (ambulance) kutupeleka Hospitali ya Taifa Muhimbili...”

“Ingawa sijawahi kupanda gari la aina hiyo tangu nizaliwe, lakini nikiwa mule niliona tayari nimenusurika kifo,” alisema kijana huyo.

Kuhusu hatma ya mtaji wake, Yahaya alisema bado hajatulua kuweza kupiga hesabu rasmi kujua kiwango cha hasara kutoka kwenye janga hilo ambapo alikuwa na mtaji wa zaidi ya shilingi milioni 40.

Mtaji wake anasema kuwa ulikuwa zaidi ya milioni 40, ikiwa ni pamoja na fedha taslimu zilizokuwamo ndani ya duka lake hadi siku ya tukio.

Kuhusu uwezekano wa kunusuru baadhi ya mali zake zilizokuwa kwenye jengo hilo, Yahaya amesema kuwa hana uhakika nini kitafuata.

“Kwa sasa nakubaliana na uhalisia, najua mtaji wangu umeondoka, sasa hivi ninachoweza kufanya ni kuanza upya, nitaanzia pale nilipoishia kidogo kidogo nitanyanyuka kwa sababu sina mkopo benki,” alisema.

Aidha, mfanyabiashara huyo amesema haamini kama jengo lililoporomoka lilijengwa chini ya kiwango, isipokuwa ni makosa yamefanyika katika uboreshaji wa sehemu ya chini.

Kwamba waliokuwa wanafanyia ukarabati eneo hilo ambalo halijawahi kutumika ndiyo waligusa kwenye maeneo yaliyokuwa ameshikilia jengo hilo.

Amesema jengo hilo lina umri wa miaka 12 tangu lijengwe, lakini sehemu ya chini ili-

kuwa haitumiki, hivyo waliokuwa wanafanyia ukarabati ili lianze kitumika huenda waligusa maeneo ambayo yalikuwa yameshikilia jengo lote.

“Inawezekana kabisa mafunzi waliokuwa wakifanya kazi eneo la chini waligusa nguzo ambayo ilikuwa imeshikilia jengo zima na kuwa sababu ya kuporomoka kwake,” amesema.

Kijana mwingine, Massawe hakuwa na maneno mengi ya kuzungumza zaidi ya kumshukuru Mungu na kusema kuwa licha ya kuponea chupuchupu kupoteza uhai wake, anaipenda Kariakoo kwani ni sehemu yake muhimu ya kujipatia riziki.

“Wakati jengo linaanguka nilisikia kitu kama mtikisiko hivi, sekunde chache tu tukajikuta tumefunikwa. Wenzetu waliokuwa nje walifanya juhudi kubwa kufanikisha kupona kwetu,

“Licha ya madhila haya, siwezi kusema nina mpango wa kuondoka Kariakoo, hapa Kariakoo nipo sana tu, sasa hivi namsikiliza bosi wangu atasema nini kuhusu hatma ya mtaji na mali zilizopotea kwenye janga hili,” amesema.


Jengo hilo la ghorofa tatu lilianguka Jumamosi Novemba 16 ambapo mpaka sasa watu 26 wametajwa kufariki dunia katika mji mkuu wa kibiashara wa Dar es Salaam.

Hadi Jumamosi Novemba 23 shughuli za uokozi zilikuwa zinaendelea katika eneo hilo, ambapo Pambazuko lilishuhudia magari kadhaa yakibeba kifusi kutoka kwenye eneo hilo, ingawa taarifa hazijawekwa wazi endapo bado kuna watu walio hai au miili iliyonasa kwenye jengo hilo.

Alipotembelea eneo hilo Jumatano, Novemba 20, 2024, Rais Samia Suluhu Hassan alisema serikali haitasita kubomoa majengo yote ya Kariakoo iwapo tume iliyoundwa kuchunguza usalama wake, itashauri ifanyike hivyo.

Sambamba na hilo, mkuu huyo wa nchi amewasihi watendaji wa serikali kuwajibika kwa nafasi zao, hasa katika mchakato wa utoaji vibali vya ujenzi akitaka visimamiwe.

Rais aliagiza iundwe tume kuchunguza majengo yote ambapo tayari Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ameiunda ikiwa na wajumbe 19, akibainisha kuwa matokeo yatakayopatikana yatawekwa wazi kwa wananchi.



Marekani



Utata kesi jinai za Trump baada ya ushindi



Rais Mteule wa Marekani, Donald Trump.

Na Mwandishi WETU

MSHINDI wa uchaguzi wa urais nchini Marekani, Donald Trump, aligombea nafasi hiyo akiwa anakabiliwa na kesi kadhaa mahakamani.

Baadhi ya kesi hizo ni za jinai, zikihusiana na matukio ya Januari 2020 alipowahamasisha wafuasi wake kupinga kwa nguvu matokeo ya uchaguzi yaliyompa ushindi Joe Biden.

Wafuasi hao wakavamia jengo nyeti lenye ofisi muhimu za serikali la Capitol na kufanya uharibifu pamoja na kujeruhi. Askari mmoja alipoteza maisha katika purukushani hizo.

Tuhuma nyingine zinahusiana na masuala ya

kodi, matumizi mabaya ya fedha na kughushi au kuficha takwimu za malipo ya fedha.

Katika moja ya kesi hizo kuhisiana na malipo ya fedha tayari mahakama ilishamkuta Trump na hatia ya kudanganya takwimu za biashara na kinachosubiriwa dhidi yake ni hukumu tu.

Hali hii imezua utata kidogo kwa sababu hii ni mara ya kwanza kwa mtu ambaye ameshakutwa na makosa mahakamani kuchaguliwa kuwa Rais wa Marekani.

Sasa hivi haijulikani wazi ni nini kitatokea kuhusiana na kesi hizo zinazomkabili Trump.

Katika kampeni Trump alishaahidi kuwa akishinda atamtimua mwendesha mashitaka Jack Smith ili kumaliza kesi kadhaa ambazo amezifungua dhidi yake kuhusiana na matukio ya uchaguzi wa 2020.

Sasa hivi inaonekana mahakama imeamua kuzichelewesha kesi hizo ili kujipa muda wa kutafakari.

Jaji mmoja jijini New York ameamua kufuata ushauri huo kwani ameahirisha kwa muda usiojulikana tarehe ya kutoa hukumu dhidi ya Trump. Hukumu hiyo ilipangwa kusomwa baadaye mwezi huu, baada ya kuahirishwa awali.

Jaji huyo aliahirisha hukumu hiyo awali kwa maelezo kuwa hakutaka kuingilia uchaguzi mkuu uliokuwa unaendelea.

Trump alipaswa kufika mahakamani kesho Novemba 26 ili kusikiliza hukumu dhidi yake baada ya kukutwa na hatia katika makosa 34 ya kughushi rekodi za biashara ili kuficha uhalifu wa kifedha alioufanya mwaka 2016.

Mwaka huo, wakati akigombea urais, Trump alilazimika kumlipa nyota wa filamu za ngono, Stormy Daniels, kama njia ya kuzima kashfa iliyokuwa inamwandama na kuhatarisha kampeni zake.

Mawakili wa Trump wamekuwa wakitaka kuchelewesha kesi hiyo tangu wakati ilipoanza kusikilizwa. Hivyo, uamuzi wa kuchelewesha hukumu hiyo litakuwa ni jambo zuri kwao.

Lakini inaelekea kuwa sasa, baada ya bosi wao kushinda urais, kampeni zao zitajikita kwenye kuhakikisha kuwa kesi hiyo inafutwa kabisa.

Inaendelea Uk. 17



Utata kesi jinai za Trump baada ya ushindi

Inatoka Uk. 16

Inaaminika kuwa mawakili wa Trump wataieleza mahakama hiyo kuwa kama Rais Mteule, Trump ana haki ya kulindwa na kati-ba kama kiongozi mkuu wa nchi na anapaswa kulindwa dhidi ya mashitaka ya aina yoyote kutoka kwa waendesha mashitaka wa serikali.

Lakini iwapo jaji atashikilia msimamo wake wa kumkuta Trump na hatia, mawakili wa rais huyo wa zamani wamepanga kumuomba jaji huyo kuchelewesha utoaji wa hukumu hiyo ili wakate rufaa.

Baada ya kumkuta Trump na hatia, jaji huyo alitoa fursa kwa pande zinazovutana kwenye kesi hiyo kutoa maelezo yao ya mwisho kwa maandishi kabla hajatoa hukumu. Alipanga maelezo hayo yawe yameshatolewa ifikapo katika ya mwezi huu.

Katika maelezo yao mawakili hao wameomba hukumu ya kesi hiyo icheleweshwe. Na kama mawakili wa Trump wakifanikiwa kupata fursa hiyo ya kukata rufaa, basi wamepanga kutumia hoja ya ulinzi wa kiongozi wa nchi dhidi ya mashitaka ya jinai, ili kuishawishi mahakama ya juu iifute kesi hiyo.

Iwapo jaribio hilo likishindwa, kwa makosa aliyokutwa nayo, Trump anaweza kuhukumiwa kifungo cha miaka minne gerezani.

Pia katika hoja zao wamepanga kuhoji iwapo jaji wa mahakama ya jimbo ana mamlaka ya kumhukumu Rais Mteule.

Hata hivyo, sheria haimbani Jaji kutoa hukumu hiyo ya kufungwa jela kwa Trump na anaweza kutoa hukumu nyepesi, kama vile kuwekwa chini ya uangalizi kwa kipindi fulani, kifungo cha nyumbani au kufanya kazi za kijamii au hata kulipa faini.

Hata hivyo, hukumu yoyote itakayotolewa itakuwa na ugumu kuitekeleza kwani Trump anatarajiwa kuanza kushika nafasi ya rais Januari 20 mwakani.

Lakini kwa upande mwingine, kwa kuwa kesi hiyo imefunguliwa katika mahakama ya jimbo, Trump hatakuwa na mamlaka ya kujipa

msamaha mwenyewe hata baada ya kuapishwa mwakani na kuwa Rais.

Mamlaka hayo anaweza kuyatumia kwenye kesi za mahakama kuu peke yake.

Ushindi wa Trump pia unaleta utata katika kesi nyingine mbili za jinai zilizofunguliwa dhidi yake mahakama kuu katika majimbo ya Washington na Florida.

Kesi hizo zilifunguliwa 2023 na mkakati mkubwa wa Trump tangu wakati huo ulikuwa ni kuzichelewesha kesi hizo kadri ilivyowezekana.

Hilo limefanikiwa kwa kiasi, kwani kesi zili-cheweshwa hadi uchaguzi ulipofanyika.

Smith ndiye anazimimamia kesi hizo na mwezi uliopita, wakati wa kampeni, Trump aliahidi kuwa akishinda atamfuta kazi mwendesha mashitaka huyo.

“Ni jambo rahisi sana,” Trump alisema alipoulizwa atajipatia msamaha yeye mwenyewe akiwa rais iwapo atapatikana na hatia katika kesi hizo. “Ni kufukuza kazi tu huyo Jack Smith iwapo nitachaguliwa. Nitamtimua sekunde mbili baada ya kushinda,” alisema Trump.

Wakati huohuo maofisa wa Wizara ya Sheria wanaangalia jinsi ya kuzimaliza kesi hizo mbili bila kupingana na maelekezo ya ofisi ya Mwanasheria Mkuu yaliyotolewa 2020 kuhusiana na kumshitaki rais aliyepo madarakani.

Watu walio karibu na Smith, wakiwemo wafanyakazi wa ngazi za juu kutoka Wizara ya Sheria, wanasema kuwa Smith hana mpango wa kutoa upendeleo wowote na kuifuta kesi hiyo, hata kama msimamo huo utamgharimu ajira yake na kutimuliwa na Trump.

Katika kesi iliyoko New York, Smith anamshitaki Trump kwa tuhuma za kulazimisha kupinduliwa kwa matokeo ya uchaguzi wa 2020.

Kesi hiyo ilicheleweshwa kwa miezi kadhaa wakati mawakili wakitaka Trump apatiwe kinga ya kutoshitakiwa kama rais mstaafu.

Julai mwaka huu mahakama kuu ilitoa hukumu ya kihistoria ikisema kuwa katika masuala kadhaa rais huyo mstaafu ana kinga ya kutoshitakiwa kwa makosa ya jinai.



Na Mwandishi WETU



Uchumi & Biashara

Kukopesha simu kwanufaisha Vodacom

Na Mwandishi WETU

WAFANYABIASHARA wanaokopesha simu za viganjani wameongezeka zaidi, hasa katika miji mikubwa nchini Tanzania.

Mpango huo wa kukopesha simu ume-wawezesha Watanzania wengi wenye kipato cha kawaida kumiliki simu janja huku wakilipia kwa awamu.

Wengi wanadhani kuwa huo ni mpango wa wafanyabiashara kujiongezea mauzo, bila kujua kuwa ni mpango uliobuniwa na kuanzishwa na kampuni kubwa za simu za mikononi, Vodacom Tanzania ikiwamo.

Katika ripoti yake ya mwaka ulioishia Septemba mwaka huu, Vodacom Tanzania imeripoti kuwa mpango huo wa kuuza simu kwa mkopo ni moja ya mikakati ambayo imesaidia kuongeza mafanikio ya kampuni hiyo katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita.

Ripoti hiyo, inaeleza kuwa moja ya sababu zilizopaisha mapato ya kampuni hiyo ni kuongezeka kwa wateja wanaotumia simu janja, ambao idadi yao imeongezeka zaidi mwaka uliopita kutokana na mpango wa kuuza simu hizo kwa mikopo.

“Idadi ya watumiaji wa simu janja katika mtandao wetu iliongezeka kwa asilimia 23.6, ikisaidia ukuaji wa karibia asilimia 50 wa matumizi ya data za 4G,” inasema ripoti hiyo ya Vodacom Tanzania.

Aidha, ongezeko hilo la idadi ya wateja wa simu janja kuliisaidia kampuni hiyo kukuza mapato yatokanayo na matumizi ya data kwa asilimia 16.3 katika robo ya pili ya mwaka.

Ukuaji mkubwa

Mapato yameongezeka, idadi ya wateja imeongezeka, faida imeongezeka, matumizi ya data na sauti yameongezeka.

Hali hii inathibitisha mwenendo mzuri wa kampuni ya simu za kiganjani ya Vodacom katika kipindi cha mwaka ulioishia mwishoni mwa Septemba mwaka huu.

Ripoti iliyochapishwa na kampuni hiyo

hivi karibuni inaonyesha kuwa mapato yake ya huduma yaliongezeka kwa asilimia 19.1 na kufikia shilingi bilioni 718.2 katika kipindi hicho.

Kukua huko kwa mapato, inasema kampuni hiyo, kumetokana na kuimarika kwa biashara zake nchini Tanzania.

Kwa upande mwingine, kampuni hiyo imebainisha kuwa idadi ya wateja imeongezeka kwa asilimia 13.2 na kuiwezesha kufikia wateja milioni 20.9 kati ya watumiaji wa simu za viganjani nchini.

Ongzeko hilo la wateja na jinsi walivyou-tumia mtandao huo kupata huduma mbalimbali kulichangia pia kuongezeka pia kwa wastani wa mapato kwa mteja kwa asilimia 1.9 katika mwaka husika.

Katika kipindi hicho Vodacom ilivuna kiasi cha shilingi bilioni 153.5 kutoka kwa wateja wake waliotumia huduma za sauti, likiwa ni ongezeko la mapato ya kitengo hicho kwa asilimia 8.6 kwa mwaka.

Katika robo ya pili, Vodacom inasema, mapato ya huduma za sauti yaliongezeka kwa asilimia 6.3, mapato kutokana na huduma za M-Pesa nayo yakakua kwa asilimia

27.9 na kufikia shilingi bilioni 274.2 na kuongeza mchango wake katika pato la kampuni na kufikia asilimia 38.2.



Mkuu wa Idara ya Mauzo na Usambazaji wa Vodacom Tanzania, George Lugata akionesha simu ambayo mteja wa kampuni hiyo anaweza kuimiliki kwa kulipa kidogokidogo. Kushoto ni Mkurugenzi wa D.Light Tanzania, Charles Natai. (Picha na Maktaba)



Mchumi aipa TRC maua yake

Na Hellen NGOROMERA

MTAALAMU wa Uchumi na Fedha kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) Profesa Haji Semboja, amesema ana imani na Shirika la Reli Tanzania (TRC) litajitania zaidi.

Akizungumza na Pambazuko baada ya TRC kutangaza kuwa tangu kuanza kwa huduma za treni ya kisasa inayotumia umeme (SGR) tayari imesafirisha abiria milioni moja.

Hivi sasa ni mikoa ya Dar es salaam, Pwani, Morogoro na Dodoma ndiyo inanufaika na huduma za treni hiyo ya kisasa.

Prof. Semboja amesema pamoja na SGR kuanza kutoa huduma, lakini bado haijafika mikoa ya Mwanza na Kigoma, njia ya Kaskazini na Kusini.

“Lakini tunatarajiwa kuwa baada ya kukamilisha kusambaza huduma nchini reli hiyo sasa itafikishwa kwenye nchi jirani tukianzia na Afrika Mashariki na baadaye nchi za SADC na kasha kujisambaza hadi Afrika ya Kati,” amesema.

Kwa mujibu wa Profesa Semboja, SGR ni mradi mkubwa na ndio maana utekelezaji wake umegawanywa kwa awamu.

Amesema juhudi za TRC ni za kuungwa mkono kwani mafanikio makubwa ya mradi huo yataanza kuonekana TRC itakapoanza kutoa huduma ya kusafirisha mizigo kupitia reli hiyo.

Hivi karibuni TRC ilisema tangu kuanza kwa usafiri huo Juni mwaka huu, tayari imesafirisha abiria milioni moja.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa TRC, Fredy Mwanjala, amesema kuwa idadi hiyo ni mara mbili ya abiria waliokuwa wakisafiriswa kwa treni ya zamani (MGR) ambayo ilisafirisha jumla ya abiria 400,000 katika kipindi cha mwaka mmoja.

Sambamba na hilo, TRC imetangaza kuku-sanya shilingi bilioni 20 katika kipindi hicho.

Alisema TRC inatambua umuhimu wa huduma hiyo ya kisasa katika kuboresha usafiri, kuongeza ufanisi wa biashara na kutoa chaguo la haraka na salama kwa abiria.

Mwanjala aliwashukuru Watanzania kwa kuunga mkono jitihada za TRC kuboresha usafiri wa treni za mwendokasi zinazotumia nishati ya umeme na kuwahakikishia kuwa wataendelea kutoa huduma bora zaidi kwa abiria.



Rais Samia Suluhu Hassan, wa pili kushoto akiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi mbalimbali wakati wa mkutano wa G20 uliofanyika hivi karibuni nchini Brazil. (Picha na Ikulu)

Maombi ya Rais Samia kwa matajiri G20

Na Mwandishi WETU

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan amejua kutumia fursa ya kukutana na matajiri wa dunia – katika mkutano wao uliomalizika Brazil wiki iliyopita.

Katika mkutano huo, na mikutano mingine ya pembeni, Rais Samia aliomba kuungwa mkono na nchi kusaidiwa kwenye masuala anuai; matumizi ya kani rafiki, kilimo cha kisasa na teknolojia.

Rais Samia alialikwa kwenye mkutano mkubwa wa G20, uliofanyika nchini Brazil, Novemba 18 na 19 mwaka huu.

Alikuwa miongoni mwa viongozi waliohutubia katika mkutano huo unaofanyika kila mwaka na kuzikutanisha nchi 20 zenye nguvu kiuchumi zinazochangia zaidi ya asilimia 85 ya pato la dunia (GDP).

Baada ya kumalizika mkutano huo, Rais

Samia alizungumza na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari ambapo pamoja na mambo mengine, alisema hatua ya Tanzania kushiriki kwenye mkutano huo ina manufaa makubwa.

Alisema katika mkutano huo, walijadili mambo makuu matatu ikiwepo kuondoa njaa, matumizi ya dizeli kwenda nishati jadidifu, utawala bora na utawala wa sheria.

Akizungumzia kuhusu njaa, alisema; “Ilikuwa ni kujadili ni kwa kiasi gani dunia imeweza kuondoa njaa ambayo ni SDG ya kwanza katika yale malengo ya milenia...”

“Sasa tulikuwa tunafanya tathmini kwa kiasi gani dunia imeweza kuondoa njaa...bado kazi haijafanyika vizuri kwa sababu kuna watu wengi duniani bado wana matatizo ya njaa na siyo Afrika peke yake, lakini na maeneo mengine tofauti...”

Inaendelea Uk. 21



Maombi ya Samia...

Inatoka Uk. 20

“Sasa katika kulizungumza hili, nchi nyingi zimetoa mikakati ya nini tufanye ili kupunguza njaa, lakini kuna zile ambazo hali zao ni nzuri, wametoa matumaini na ahadi kusaidia kifedha, kiufundi, teknolojia na mambo mengine ili kuondosha njaa,” alisema.

Alisema alipotakiwa kuizungumzia Tanzania kuhusu hoja hiyo ya chakula, aliweka wazi kwamba endapo hakutakuwa na matukio ya mabadiliko ya tabianchi, basi nchi itajitosheleza na chakula kwa asilimia 128.

“Na nikaeleza bayana kabisa kwamba tunaweza kuwauzia wenzetu, lakini tuna uwezo wa kuzalisha zaidi na kulisha nchi jirani, bara la Afrika na hata nchi za nje,” alisema.

Katika mahojiano hayo na wahariri wa vyombo vya habari, Rais Samia alisema kuwa, aliwaeleza wakuu hao wa nchi hizo tajiri kwamba pamoja na Tanzania kujitosheleza kwa chakula, lakini kuna vikwazo ambavyo ikisaidiwa kuvitatuwa inaweza kuzalisha zaidi.

Alitaja kikwazo cha kwanza kuwa ni masuala ya tafiti za kilimo, kilimo cha kisasa cha kutumia mashine na kilimo cha umwagiliaji.

“Kikwazo kingine kwenye kilimo ni mbolea; kwa muda mrefu tumekuwa tukinunua mbolea kutoka nje, kazi yetu sasa ni kuvutia wawekezaji wa viwanda vya mbolea kuja kuweka ndani, halafu tuweze kuzalisha na kusambaza kwa wakulima wetu,” alisema Rais Samia.

Alisema jambo la pili lililozungumzwa sana kwenye mkutano huo mkubwa ni matumizi ya dizeli kwenda nishati jadidifu.

“Sisi wengine bado tuko kwenye dizeli na asilimia 60 ya umeme wetu ni wa gesi, sasa wamepiga kelele tusitumie gesi, lakini tumeomba watupe muda zaidi...”

“Katika hoja hiyo kingine ni nishati safi ya kupikia na kuwataka watuunge mkono (kwa kuhakikisha) kwamba watu wengi Afrika wanapata umeme, lakini ifike wakati wananchi wetu waweze kupika kwa kutumia umeme,” alisema.

Kuhusu hoja ya utawala bora na utawala wa sheria, Rais Samia alisema; “sisi wengine katika

hoja hii tukawa wasikilizaji tu na yaliyosemwa mle ni haja ya kuona ulimwengu unakuwa salaama, haja ya kusimamisha vita vinavyoendelea, haja ya kutoa njia ya kusaidia wale waliofikwa na maafa ya vita kwamba imetosha.”

Vilevile alisema Watanzania siyo maskini kwa kuwa kuna rasilimali za kutosha, isipokuwa kuna kasoro ndogo tu za kutumia rasilimali hizo kwa lengo la kumnufaisha kila Mtanzania.

Aidha, alisema baada ya mkutano huo, alipata fursa ya kukutana na viongozi wa nchi mbalimbali na wakuu wa taasisi za kimataifa ambapo walijadili ushirikiano uliopo, miradi na maeneo mapya ya uwekezaji.

Alitaja baadhi ya viongozi aliokutana nao kuwa ni Waziri Mkuu wa Norway, Helen Clark, ambaye walijadili kuhusu ajenda ya nishati safi ya kupikia.

Wengine ni Rais wa Misri, Abdel Fattah al-Sisi ambapo walijadili mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere (JNHPP) huku Waziri Mkuu wa Vietnam, Pham Minh Chinh wakijadili kuhusu ushirikiano katika sekta ya mawasiliano. Pia alisema alikutana na Rais wa Indonesia, Joko Widodo na wakajadili kuhusu ushirikiano uliopo kwenye sekta ya mafuta na gesi.

Hotuba ya Samia kwa wakuu wa G20

Awali, akitoa hotuba yake mbele ya wakuu wa mataifa hayo makubwa duniani, akiwemo Rais wa Marekani, Joe Biden, Rais wa China, Xi Jinping na wengineo, Rais Samia alisema pamoja na utajiri uliopo duniani, lakini bado Afrika kuna changamoto ya umasikini.

Rais Samia alitaja changamoto zingine zinazoikumba nchi za Afrika ni pamoja na njaa, magonjwa, utapiamlo na uzalishaji duni.

Alisema idadi kubwa ya watu, hasa vijana wanakumbana na changamoto zinazozidi kuwa mbaya kutokana na mizozo na sera za kimataifa zinazongeza uhaba wa chakula, kukandamiza ushindani na kupunguza upatikanaji wa masoko na teknolojia muhimu.

“Watu wengi bado wanasubiri ahadi ya utandawazi kutimizwa, huku wakiwa na matumaini kwamba mageuzi katika utawala wa kimataifa yataleta uwakilishi wa haki na upatikanaji wa rasilimali zinazohitajika kutokomeza umaskini...”

Makala Maalum

Uhuru wa kutembea – Ikiwa bei inaswihi



Watu wanapita kwa uhuru kuvuka mpaka wa Afrika Kusini kuingia Zimbabwe na kurudi. Hawa wanavuka Daraja la Beitbridge. Maeneo ya daraja hilo yanaaminika kuwa yenye pilikapilika nyingi zaidi kusini mwa Afrika. Hata hivyo, taratibu za kuvuka hapo kuingia ama kutoka nchi moja, siyo zilizokusudiwa na Umoja wa Afrika (AU).

Na Sihle NYATHI, Beitbridge

AFRIKA Kusini na Zimbabwe zinatenganishwa na Mto Limpopo.

Wengi wanaoingia na kutoka nchi moja kati ya hizo, wanatumia zaidi daraja katika mto huo, ingawa kuna njia zingine ambazo hazitumiki sana.

Eneo la daraja hilo - kwa kila upande, linatajwa kuwa “bize zaidi” Afrika – kwa kuwepo muingiliano wa watu, hasa Kusini mwa Jangwa la Sahara, na labda bara zima kwa ujumla.

Daraja hilo linaloitwa Alfred Beit, jina la mfanyabiashara mashuhuri wa almasi kutoka Ujerumani aliyefanikisha kuanzishwa kwa Kampuni ya De Beers kwa kushirikiana na Cecil Rhodes.

Rhodes ni mfanyabiashara kutoka Uingereza aliyefika Afrika Kusini karne ya 19 na kufanikiwa kuwa mmoja wa matajiri wakubwa duniani

kwa wakati wake.

Karibu Daraja la Beitbridge

Gazeti la The Herald, linaeleza kuwa takriban watu 20,000 huvuka daraja hili kati ya nchi hizo mbili kila siku. Idadi hiyo inaweza kuongezeka mara tatu wakati wa sikukuu za umma.

Kila msafiri, kidhahania, anatakiwa kukaguliwa na kugongewa muhuri wa nyaraka zao na maofisa wa mipakani wa pande zote mbili.

Imefahamika kuwa kwa siku za kawaida, mchakato wa kuvuka daraka – kwa kufuata taratibu za uhamiaji, huchukua chini ya saa moja.

Kwa siku za sikukuu na mwishoni mwa wiki, muda wa kufuata taratibu za uhamiaji kuvuka mpaka wa nchi hizo, huongezeka kutokana na kuwa na idadi kubwa watu wanaovuka kupitia daraja hilo.

Malori kadhaa, takriban 900 huonekana kila siku – yakiwa yamebeba vitu vingi, kuanzia mazao, vifaa vya ujenzi hadi vifaa vya uchim-baji madini.

Magari haya makubwa hayapitii hapo kutoa Afrika Kusini na Zimbabwe, bali pia huunganisha kutoka ama kwenda Zambia, Malawi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Tanzania na Msumbiji.

Hii inafanya Daraja la Beitbridge kuwa moja ya vituo muhimu vya kiuchumi katika ukanda huu.

Lakini kwa Wazimbabwe wanaoishi na kufanya kazi Afrika Kusini, kituo hiki cha mpaka kina maana kubwa zaidi; ni kiunganishi chao kikuu na nchi yao pamoja na ndugu zao.

Pesa zinatawala Kuporomoka kwa uchumi wa Zimbabwe kwa muda mrefu kumelazimisha wananchi wake zaidi ya milioni moja kutafuta “maisha mazuri” Afrika Kusini.

Licha ya maneno ya chuki kutoka kwa wanasiasa na wananchi wengine dhidi ya Wazimbabwe wanaoingia Afrika Kusini, hali hii imekuwa faida ya kiuchumi kwa Afrika Kusini.

Inaendelea Uk. 23



Uhuru wa kutembea – Ikiwa bei inaswihi



Inatoka Uk. 22

Utafiti uliochapishwa kwenye jarida la Strategic Review for Southern Africa lilionyesha kuwa wahamiaji wanaweza kuchangia pato la taifa la Afrika Kusini kwa asilimia zinazofikia tano.

Hii inatokana na kufanya kazi mbalimbali ama biashara ambazo huwalazimu kulipa kodi kwa serikali. Pia wanaponunua bidhaa huchangia pato la Afrika Kusini.

Viza kuingia Afrika Kusini

Kuna aina mbalimbali za visa zinazowaruhusu Wazimbabwe kuishi na kufanya kazi ndani ya mipaka ya jirani zao- Afrika Kusini.

Kila anayevuka mpaka kuingia Afrika Kusini, hulazimika kuwa na pasipoti ambayo lazima ipate muhuri kuruhusu kuendelea na safari.

Hata hivyo, utekelezaji wa kugonga viza siyo thabiti, na mara nyingine hubadilika ghafla. Siyo kila mtu anayefuzu. Wapo wanaozuiwa kuingia Afrika Kusini.

Wageni wengi wanaoingia kutoka Zimbabwe huingia Afrika Kusini kwa ajili ya kufanya kazi za ndani na hawa hupewa viza ya siku 90

tu (miezi mitatu), hivyo kuwalazimu kuinga na kutoka kabla ya muda huo kumalizika.

Mfano ni Sylvia Jakachira kutoka Zimbabwe ambaye anafanya kazi za ndani katika Jiji la Johannesburg. Huyu hulazimika kusafiri kati ya mji huo na Harare; Mji Mkuu wa Zimbabwe - kila baada ya miezi mitatu.

Kazi za ndani hazichukuliwi kuwa za ujuzi maalum, ndiyo maana Afrika Kusini, haiwezi kumpa Sylvia viza ya muda mrefu.

Wajiri wake, wakitumia hadhi yake ya kuwepo Afrika Kusini, humlipa ujira mdogo – lakini anasema ni bora zaidi kuliko kukaa nyumbani Harare bila kazi.

Sheria za Afrika Kusini zinawaruhusu Wazimbabwe kutembelea nchi hiyo kwa siku 90 bila viza maalum. Hii, hata hivyo, inategemea uamuzi wa maofisa wa mpakani, na safari za “nenda-rudi” haziwapendezi maofisa hao. Hivyo, mara nyingi hugoma kugonga muhuri (viza).

Ili kukwepa hali hii, Sylvia anasema hulipa kati ya R100 na R300 (takriban Sh. 15,000 – 45,000) kila safari ili kupata muhuri unaohitajika kwenye pasipoti yake. R- ni alama ya fedha ya Afrika Kusini ikiitwa Rand.

Safari yake kuelekea mpakani, kama ya wengi wengine, huanzia katika Kituo cha Mabasi cha Powerhouse katikati ya Johannesburg.

Hapa ndipo mahali pa kupanda basi, hakuna maswali yanayoulizwa, na waendeshaji mabasi wana ujuzi wa kushughulikia usumbufu wa maofisa wa mipakani. Kuna sheria moja: “Vapeyi mari tiende” – wape pesa ili tuendelee.

“Randi mia hapa, nyingine mia pale, hakuna anayehitaji maelezo, mradi kuna pesa, hapana chekutya; hakuna cha kuogopa,” anasema Bernard Katadza, mhudumu wa basi aliyezungumza na gazeti la The Continent.

Kawaida, baada ya kusimama kwa muda mfupi Pretoria kukusanya abiria zaidi, kondakta husimama katikati ya basi kuelezea jinsi safari itakavyokuwa.

“Kutakuwa na kituo kimoja tu zaidi – mapumziko ya dakika 20 kwenye kituo cha mafuta cha Sasol mjini Musina – kisha basi litaelekea mpaka wa Beitbridge...”

Inaendelea Uk. 25



Mtoto wa Mvuvi

Na Maregesi PAUL



Hili la Kariakoo ni funzo. Poleni Watanzania



Jengo lililoporomoka Kariakoo hivi karibuni

POLENI sana Watanzania wenzangu. Nawapa pole Watanzania wote popote mlipo bila kujali makabila yenu, dini zenu na maeneo mnakoishi iwe mijini au vijijini.

Ndiyo, nawapa pole kwa sababu nchi yetu imetikisika kweli kweli. Haikutikisika kwa sababu imesukumwa na pande la mtu kutokea mashariki, magharibi, kusini au kaskazini, bali imetikisika baada ya jengo la ghorofa kuanguka na kuua makumi ya watu katika eneo la Kariakoo, Dar es Salaam.

Jengo hilo siyo la kwanza kuanguka hapo Kariakoo, siyo la pili kuanguka Dar es Salaam na pia jengo hilo ambalo liliporomoka majira ya asubuhi, siyo la nne kuporomoka, bali ni mwendelezo wa majengo mengi yaliyokwisha aanguka jijini Dar es salaam na kusababisha madhara makubwa ikiwamo kupoteza maisha ya wenzetu.

Kwa wale ambao hawajawahi kufika jijini Dar es Salaam au ambao wanaishi Dar es Salaam, lakini hawaifahamu Kariakoo vizuri, basi waelewe kwamba Kariakoo ndilo eneo maarufu la kibiashara hapa Tanzania na ndiko kilipo ki-

ini cha ukusanyaji wa mapato kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Kwa maana hiyo, tukio kama la kuanguka jengo kubwa likitokea katika eneo la Kariakoo, moja kwa moja litakuwa limeitikisa nchi kwa sababu biashara zinasimama kwa muda na hivyo kuiathiri makusanyo ya mapato.

Wapo wanaowalaumu wahandisi waliosimamia ujenzi wa jengo hilo, wapo wanaomlaumu mmiliki wa jengo lililoanguka na wengine wanailaumu Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB), kwamba imeshindwa, kwa muda mrefu kusimamia ujenzi wa majengo na hivyo kusababisha madhara kadhaa kwa watu wasiokuwa na hatia.

Hayo yamepita, kilichobaki sasa ni serikali kuchukua hatua itakazoona zinafaa ili waliokiuuka utaratibu wakati wa ujenzi wa ghorofa hilo na majengo mengine yanayoweza kusababisha madhara kama yaliyoshuhudiwa wiki iliyopita, wachukuliwe hatua zinazostahili.

Kulaumiana hakutaponya chochote. Lakini kuchukua hatua madhubuti kutatuhakikishia kuwa kile kilichotokea majuzi hakitokei tena, au kama kikitokea basi inakuwa ni kwa kudura za Mungu na siyo uzembe wa binadamu.

Katika kushughulikia tukio hilo, serikali isimuonee huruma mtu yeyote aliyechangia kwa namna yoyote kuifikisha sekta ya majengo mahali ilipo kwani tukio hilo limeionyesha serikali kwamba kuna mahali panavuja na panastahili kuzibwa haraka iwezekanavyo.

Walioshindwa kutimiza wajibu wao kupitia CRB wachukuliwe hatua wanazostahili, walioshindwa kuzifanyia kazi ripoti zilizopita kuhusu ujenzi wa majengo ya Kariakoo na kwingineko nchini, wasifumbiwe macho na wote waliotoa vibali vya majengo katika mazingira yenye utata, nao wawajibishwe bila huruma.

Pamoja na yote hayo, naamini serikali itakuwa makini katika kufuatilia tukio hilo na kua-mua kuchukua hatua bila kulindana kama ilivyo kawaida yetu.

Serikali itajua mambo mengi yaliyojificha na yanayochangia kwa kiasi kikubwa maghorofa ya Dar es Salaam kuporomoka ikilinganishwa na mikoa mingine nchini.



Uhuru wa kutembea – Ikiwa bei inaswihi

Inatoka Uk. 23

“Kwa abiria wenye nyaraka zinazotia shaka, huu ndiyo wakati wa kutuambia ili safari iendelee vyema, ieleweke kuwa fedha hulainisha mikono, gharama ni R400 (Sh. 60,000) kwa mtu aliyepitiliza muda wa viza ya siku 90; mara mbili ya kiasi hicho kwa mtu asiye na nyaraka kabisa; na R1,000 (Sh. 150,000) kwa mzazi anayesafiri peke yake na mtoto bila hati muhimu,” amesema Bernard.

Wiwango hivi ni vya kujadiliana. Abiria hawalipi moja kwa moja kwa maofisa wa mpakani.

Kwenye mpaka, abiria wote hutakiwa kushuka kutoka kwenye basi na kupanga foleni katika ukumbi usio na kiyoyozi. Joto ni kali mno, kuna mbu wamesambaa. Hali ni mbaya.

Kuna foleni moja ndefu ya kuwafikia waofisa wa Uhamiaji kwa kila basi – abiria wa kwanza kufika dirishani hupata kuhudumiwa haraka.

Siku hizi, kufuatia kukamilika mwaka 2023 kwa mradi wa ukarabati wa miundombinu wa Dola milioni 300 (Sh. bilioni 80) katika mpaka huo, upande wa Zimbabwe, mchakato huu wa kuhudumia wageni kwa kawaida hukamilika ndani ya saa moja.

Hata hivyo, Afrika Kusini wala Zimbabwe hawajaanza kutumia itifaki ya Umoja wa Afrika ya mwaka 2018 ambayo inahusu uhuru wa watu kuvuka mipaka. Itifaki hii inawapa raia wa Afrika haki ya kuishi na kufanya kazi katika nchi yoyote mwanachama bila viza.

Hata hivyo, uchumi usio rasmi wa Beitbridge unaonekana kufikia hitimisho sawa, ingawa mwendo siyo huru kabisa. “Vapeyi mari tiende.”

Kwenye uzio

Mwezi Agosti, mwaka huu, Carte Blanche, kipindi cha habari za uchunguzi cha Afrika Kusini, kilirekodi video ya raia wa Zimbabwe wakihonga maofisa wa Idara ya Uhamiaji wa Afrika Kusini ili kupata muda wa ziada wa kuishi humo.

Hili halikumshangaza Michael Masiapato, Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Mpaka wa

Afrika Kusini, aliyekiambia kipindi hicho kuwa; “Jambo moja ambalo hatuwezi kukanusha ni hali halisi ya ufisadi.”

Masiapato alisema idara yake inayosimamia vituo 71 vya mpakani nchini Afrika Kusini, ina uhaba mkubwa wa wafanyakazi.

Kwenye Daraja la Beitbridge, anaeleza kuwa anaweza kupeleka maofisa 10 tu kwa zamu, hivyo kuwepo kwa teknolojia ya kisasa, kama rekodi za kidijitali, drones za uangalizi, na kamera za mwili, kunaweza kumaliza ama kupunguza tatizo hilo.

Zinapopelekwa, teknolojia hizi zitawaruhusu maofisa wake kufuatilia wasafiri kwa ufanisi zaidi – na kumruhusu yeye kufuatilia maofisa wake.

Mamlaka zimekuwa zikihangaika - kwa muda mrefu, kudhibiti mwendo wa watu kuvuka Mto Limpopo kwa kuhonga maofisa wa Uhamiaji.

Wakati wa utawala wa kibaguzi wa wazungu ulijenga uzio wa umeme kando ya sehemu kubwa ya mpaka, na kupiga doria kwa umbali wa kilomita 233 kwa askari na mbwa ili kuzuia wapigania uhuru kuingia na wengine kutoka nchini humo.

Katika kipindi hicho, wapigania uhuru wa wengi Afrika Kusini walikuwa kwenye nchi za Zimbabwe, Zambia, na Tanzania.

Makaburu hao hata hivyo, hawakufanikiwa sana, ndipo waliopoamua kuleta kundi la mbwa mwitu – ndiyo, mbwa mwitu – kutoka Amerika Kaskazini na kuwafuga ili kuwinda waasi.

Mpango huo pia ulishindwa. Kwani watu walibuni mbinu nyingine za kuingia na kutoka Afrika Kusini.

Miaka ya hivi karibuni, Afrika Kusini – ikiwa chini ya uongozi wa kidemokrasia, ilitumia zaidi ya \$2 milioni (Sh. bilioni 5.3) kuimarisha uzio sehemu za mpaka. Uimarishaji huo haukudumu muda mrefu.

Uzio huo uliharibika na hata kutoweka kabisa maeneo fulani, na sasa unadhihakiwa kama “kamba ya kuanikia nguo ya Beitbridge.”

Mavazi ya watoto yaliyoachwa na mabegi mabovu yaliyokamatwa kwenye maeneo ya mmpaka huo yanaonekana yakining’inia kwenye nyaya za uzio huo.

Inaendelea Uk. 31

 Kenya

Besigye kutekwa Nairobi doa kwa serikali ya Ruto

Na Julius MKAMBI

Tukio la hivi karibuni linalohusisha kutekwa kwa kiongozi wa upinzani kutoka Uganda, Dkt. Kizza Besigye, akiwa nchini Kenya na baadaye kuibukia kwenye mahakama ya Kijeshi nchini kwao, kumeifanya serikali ya Rais William Ruto kumulikwa tena.

Malalamiko yamekuwa mengi kutoka kwa raia, mashirika yasiyo ya kiserikali yanayotea haki za binadamu na Chama cha Mawakili Kenya (LSK), kuitaka serikali kukabiliana na matukio haya ya utekaji nyara huku watuhumiwa wakuu wakidaiwa ni maofisa wa polisi.

Hata hivyo, katika moja ya mahojiano maalumu na vyombo vya habari, Rais Ruto alikana idara ya polisi kuwa na kitengo maalumu kinachohusika na utekaji nyara huku akiimiminia sifa idara hiyo ya jeshi la polisi kwa kudumisha usalama, hususan wakati wa maandamano ya vijana wa Gen Z.

Waliotekwa nyara na kisha kuachiwa baada ya siku kadhaa wakiwa wametupwa mbali na maeneo waliyokamatwa, walieleza madhila waliyopitia wakati wakiwa mikononi mwa watekaji hao ambao wanawataja kuwa ni maofia wa polisi.

Akihutibia Bunge Alhamisi ya wiki iliyopitia, Rais Ruto aliwataka wale wote waliyotekwa nyara kutoa taarifa polisi kwa uchunguzi zaidi.

Hotuba hiyo ya Rais alitoa siku chache tu baada ya kuibuka kwa taarifa za kutekwa kwa Besigye akiwa Nairobi na kusafirishwa hadi Uganda ambapo alipelekwas wkenye mahabusu za kijeshi hadi Jumatano iliyopita alipofikishwa katika mahakama ya kijeshi akishitakiwa na tuhuma za kumiliki silaha kinyume na sheria.

Ilikua ni afueni kwa familia ya mwanasiasa huyo wa upinzani kutoka Uganda kumuona mpendwa wao amesimama kizimbani baada ya kuripoti kutoweka kwake akiwa kwenye ziara jijini Nairobi.

Mtoa taarifa ya kutoweka kwa Besigye alikuwa mkewe, Winnie Byanyima, aliyetumia mtandao wa kijamii kushinikiza kuachiliwa kwa mumewe ambaye alisema anashikiliwa kwenye jela ya kijeshi baada ya kutekwa jijini Nairobi.

Inaendelea Uk. 27



Besigye kutekwa Nairobi doa...

Inatoka Uk. 26

Besigye alikua nchini Kenya kwa lengo la kuhudhuria uzinduzi wa kitabu kilichoandikwa na kiongozi wa chama cha Narc Kenya, Martha Karua, ambaye alikua mgombea mwenza wa Raila Odinga kwenye uchaguzi mkuu uliyopita.

Karua aliwataka Rais wa Uganda Yoweri Museveni na Rais Ruto kuelezea alipo mwanasiasa huyo wa upinzani kutoka Uganda.

Hoja hiyo ya Karua ni kama ilijibiwa na Museveni kufuatia Besigye kufikishwa mahakamani huku naye Rais Ruto kwenye hotuba yake akiwataka wanaotekwa nyara na kuachiliwa kutoa taarifa.

Siku aliyotoweka, inasemekana Besigye aliondoka hotelini saa 10 jioni akiongozana na Haji Lutale na kuelekea kwenye mkutano, wakitumia taxi.

Wawili hao waliingia kwenye chumba cha mkutano na hawakutoka tena licha ya kumwambia dereva wa taxi awasubiri hadi mkutano utakapomalizika.

Lakini walioshuhudia tukio nzima la utekaji walisema saa moja baada ya Besigye na Lutale kuwasili kwenye chumba cha mkutano, watu wasiojulikana nao pia waliwasili kwa aina ya gari linalotumika sana kwenye utekaji nyara na kuingia sehemu iliyotengwa kwa mkutano huo.

Dakika chache baada ya saa moja usiku watu hao wasiojulikana waliondoka baada ya purukushani na walinzi wa hoteli na inaaminika waliondoka na Besigye na Lutale na kusafiri hadi jijini Kampala kwa njia ya barabara.

Mashuhuda wa tukio hilo wanasema watu hao wasiojulikana hawakuonekana kama raia kutoka Kenya, hivyo kuibua maswali inakujaje watu kutoka nje ya nchi wanafanya utekaji humu nchini?

Maofisa wa Wizara ya Mambo ya Nje na wenzao wa Usalama wa Ndani wanahitajika kutoa majibu kuhusu matukio haya ya utekaji nyara sio tu kwa raia wa ndani bali sasa inaonekana

yakiwalenga wageni pia.

Tukio la kutekwa kwa Besigye akiwa Kenya limekuja takribani miezi minne baada ya raia 36 wa Uganda ambao ni wafuasi wa Chama cha Forum for Democratic Change (FDC) kinachoongozwa na kiongozi huyo wa upinzani kutekwa nyara wakiwa Kisumu na kurudishwa Uganda ambako inadaiwa kuwa waliteswa wakiwa chini ya ulinzi.

Kundi hilo lilisafiri kwenda Kenya kuhudhuria kongamano la viongozi na waliruhusiwa na maofisa wa uhamiaji wa pande zote mbili za Kenya na Uganda kuvuka mpaka.

Rais wa LSK, Faith Odhiambo, alisema kilichomtokea Besigye kinaleta picha mbaya kwa taifa na kuonekana kama nchi ambayo mtu yeyote anaweza kuja na kuvunja sheria.

Ni kauli ambayo iliungwa mkono na Karua ambaye alimtarajia Besigye kuwa moja wa wazungumzaji kwenye uzinduzi wa kitabu chake kinachoitwa 'Against the Tide' (Dhidi ya Mawimbi) akitilia wasiwasi ongezeko la matukio ya utekaji nyara, huku matukio mengine yakitekelezwa na mamluki wa kigeni.

"Watu wanatekwa nyara na maofisa wasio na sare rasmi na mamluki wa kigeni kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki," alisema Karua.

Hadi Besigye anapangwa kuwa moja wa wazungumzaji kwenye tukio la Karua la kuzindua kitabu, ni wazi aliingia nchini kwa kufuata sheria ila kinacholeta maswali ni kutekwa kwake na kusafirishwa hadi Uganda na kuibua maswali kuhusu uwezo na mamlaka ya vyombo vya usalama nchini Kenya.



Rais wa Kenya, William Ruto



Riwaya

Viaticum-16

Sakramenti ya Mwisho



Kwa wasomaji wapya: Mwandishi wa habari Eddy bado amemomaa. Aausaka ukweli wa kifo cha askofu. Anapambana huku na kule kuhakikisha anapata anachokitafuta. Je, wapi atafikia? Endelea...

Na Godwin Chilewa, Houston, MAREKANI

“Kwa nini hukuusoma?”

“Kwa sababu sikuuona, ujumbe wenyewe ameuandika kwenye mojawapo ya vipeperushi vilivyogawiwa kanisani, na huyo kijana aliponipa hakuniambia kama kuna ujumbe wowote umean-dikwa humo. Kwa kifupi sikuuona hadi niliporudi hotelini.

“Sasa kama umeshapata ujumbe wako, tatizo liko wapi?”

“Nimejaribu kumtafuta aliyeniandikia ujumbe huo bila mafanikio; na kwa bahati mbaya sina namba yake ya simu, hivyo sijui nitampataje” Eddy alisema kwa aibu kidogo.

“Kijana, ngoja nikwambie ukweli. Kama huyo unayemuita jamaa yako ni mwanamke uliyekutana naye kwenye mitandao, basi umeliwa! Tena kama ulimpa pesa zako jua umeshatapeliwa. Hutamuona kamwe?”

“Hapana katekista, mimi siyo mtu wa aina hiyo, na kama ingekuwa ni suala la mwanamke wala nisingejisumbua namna hii”

“Huyo jamaa yako anaitwa nani?”

“Sifahamu jina lake, leo ndiyo ilikuwa tuonane kwa mara ya kwanza. Kwa ufupi yeye ananifahamu, ila mimi simifahamu”

“Sasa unamtafutaje mtu usiyemjua?”

“Kwa sababu nimetumwa na mtu muhimu aliyenihakikishia kwamba mwenyeji wangu atanitambua na kunipa mzigo wake,” alidanganya.

“Sasa unataka nikusaidiaje? Katekista aliuliza huku akimungalia kwa macho makali.

“Haja yangu ni kumpata yule kijana aliyenipa kile kipeperushi. Naamini yeye anaweza kunisaidia kumpata mtu aliyempa ule ujumbe aniletee.”

“Una maana gani?”

“Nataka kumuuliza maswali machache tu ya kunisaidia kumpata huyo aliyemtuma.

“Wewe ni polisi? Au afisa usalama wa taifa?” Aliuliza kwa wasiwasi kidogo.

“Hapana, mimi ni mwandishi wa habari”

“Ninyi waandishi wa habari ni watu matata sana. Kazi yenu ni kuchokonoa mambo ya watu na kuwapaka matope. Ndiyo maana huyo mtu akakukimbia.”

“Hapana katekista, hilo siyo lengo langu na wala silo lililonileta hapa. Nina mambo muhimu zaidi ninayoweza kufanya kuliko kupaka watu matope”

“Bwana mdogo, unajisumbua bure, hao vijana unaowatafuta hawapo hapa, wameshaondoka kitambo kurudi makwao,” Katekista alisema huku akimuangalia kwa macho makali kana kwamba waligombana.

“Unawafahamu?” Eddy aliuliza kwa upole.

“Wewe siyo umesema ulikuwepo kwenye misa?”

“Naam, nilikuwepo”

“Uliwaona vijana waliotumikia?”

“Niliwaona, lakini sikukariri sura zao” Eddy alijibu huku nikijaribu kuvuta taswila ya vijana waliotumikia madhabahuni.

Walikuwa vijana sita, waliovaa kanzu za nyeupe zenye kola nyekundu. Sura zao zilikuwa zimehifadhiwa vyema kwenye ubongo wake. Lakini hiyo ingesaidia nini? Labda kama angekuwepo mtaalam anayeweza kusikiliza maelezo yake na kuwachora.

“Baada ya tangazo la msiba wale vijana waliotumikia altareni ndio waliopewa kazi ya kugawa vipeperushi. Walipomaliza majukumu yao wakachukuliwa kurudishwa kwao maana hawaishi mjini hapa”

“Wanaishi wapi? Na ilikuwaje wakaja kutu-

Inaendelea Uk. 29



Viaticum-16

Sakramenti ya Mwisho

Inatoka Uk. 28

mikia kanisani siku ya leo kama siyo wenyeji wa hapa?

“Ni vijana watumikiaji kutoka Parokia ya Bujora. Unapajua Bujora?”

“Hapana, sipafahamu.”

“Ni Kijiji kilicho nje ya Mji wa Mwanza yapata kilometa kumi na nane kama unaelekea Musoma.”

“Ilikuwaje mpaka wakaja kutumikia hapa? Kwani kanisa hili halina vijana?”

“Tunao, lakini hao walikuja kwa mwaliko wa marehemu Baba Askofu Simba. Yeye ndiye aliyeagiza waletwe kwani yeye ndiye ilikuwa aongoze misa ya watakatifu”

“Hilo nafahamu, Baba Padri alitutangazia ali poanza kuendesha misa. Sasa kwa nini askofu alitaka watumikiaji watoke Bujora?”

“Askofu Simba alikuwa akipenda sana suala la utamadunisho. Yaani kumuabudu Mungu kati ka roho na kweli pasipo kutupilia mbali mila na tamaduni za kiafrika zisizochafua imani.”

“Kwa hiyo misa ya leo kama angeiendesha baba askofu ingekuwa ya kitamaduni zaidi. Hawa vijana wangepanya vitu ambavyo hujawahi kuviona maishani. Kama hujui, Bujora ndiyo kitovu cha utamadunisho wa Kisukuma.”

“Sasa imekuwaje wameondoka mbio mbio?”

“Dereva wa gari la kukodi aliyewaleta amekuja kuwachukua. Unajua, hakuna aliyejua kama kutakuwa na msiba kwa hiyo dereva ametimiza wajibu wake.”

“Vile vipeperushi walivyogawa vilitoka wapi? Na nani aliyewapa kazi ya kuvigawa?”

“Vipeperushi vilikuwepo ofisini kwa askofu siku nyingi tu, tangu Baba Lucas Simba aliposimikwa uaskofu.”

“Kwa kifupi hatukuona sababu ya kuvitupa. Baada ya kifo chake ndipo ikaamuliwa vigawiwe kwa waumini kwa kumbukumbu yake.”

“Kina nani walioamua? Eddy aliuliza.

“Viongozi wa kanisa, sisi ni walei tu, tunapokea

maagizo toka juu.”

“Mapadre ndiyo walivileta?”

“Wao walitoa maagizo tu, masista ndiyo walio vileta na kuwapa hao vijana wawagawie waumini”

“Nakushukuru sana katekista kwa msaada wako,” Eddy alimaliza mazungumzo huku akimpa mkono.

“Ubarikiwe kijana, siku nyingine kuwa muan galifu,” Katekista alijibu huku akitabasamu.

Kufikia hapo Eddy akaona anapoteza muda wake bure. Vijana alioamini wangeweza kumsaidia walikuwa wameshaondoka, na hakuona uhusiano wowote kati ya mapadre na masista walioleta vipeperushi hivyo na mtu anayemtafuta.

Nadharia moja ilimjia kichwani. Kwamba mwenyeji wake alimuona mahali alipokuwa amesimama.

Akachukua kipeperushi kimoja, akaandika Viaticum kisha akampa yule kijana ampelekee. Pengine alifikiri Eddy angeona neno hilo mara tu baada ya kupewa kadi hiyo, na hapohapo angemuuliza yule kijana mahali pa kumpata mtu ali yempa.

Kwa bahati mbaya haikuwa hivyo.

Basi akamuaga katekista, akaondoka kuelekea yalipo maegesho ya taksi. Akiwa anaendelea kutembea simu yake ya mkononi ikatoa mlio kuashiria kuna ujumbe mpya umeingia.

Mara moja mawazo yangu yakaenda kwa Stella kwa maana ndiyemwenye kawaida ya kumtumia ujumbe wa simu mara nyingi kuliko mtu yeyote.

Akaendelea kutembea huku akiingiza mkono wa kulia kwenye mfuko wa wa suruali yake, akatoa simu, akaiwasha.

Alipoangalia kisanduku cha ujumbe wa simu akaona kuna ujumbe kutoka kwa watu mbalimbali. Kati ya hizo nne zilitumwa kwenye sanduku la ujumbe wa kawaida, na zilizobaki zilitumwa kwenye Whatsapp.

Akafunguakusoma ujumbe ulioingia wakati huo, maana ndio uliokuwa wa kwanza kwenye orodha. “Nenda kwenye nyumba ya masista, ”ujumbe huo ulijieleza kwa kifupi bila kutaja jina la mtu aliyetuma.

Haraka akaishika simu yake kwa mikono miwili, akapiga picha skrini ya simu kisha akaihi fadhi kwenye sanduku la picha zake.

Itaendelea...

Hekaheka za kampeni

Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe akihutubia mkutano wa kampeni za uchaguzi wa serikali za mitaa katika Kata ya Kabwe mkoani Mbeya mwishoni mwa wiki. (Picha na Chadema)



Mbunge wa Jimbo la Tanga Mjini (CCM), Ummy Mwalimu, akiwanadi wagombea nafasi ya uenyekiti wa Mitaa katika Kata 4 mkoani Tanga juzi.



Kiongozi wa ACT Wazalendo, Dorothy Semu akisalimiana na viongozi wa chama hicho baada ya kuwasili Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma jana. (Na Mpigapicha Wetu)



Katibu wa Itikadi, Uenezi, Siasa na Mafunzo wa CCM, Amos Makalla, akihutubia mkutano wa kampeni katika Jimbo la Kibamba eneo Kimara Stop Over jijini Dar es Salaam juzi. (Na Mpigapicha Wetu)



Katibu Mwenezi wa Chadema Kata ya Iganjo, Muhammed Mwanitwe akiwanadi wagombea wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji wa Kata ya Uyole Mbeya jana. (Na Mpigapicha Wetu)

Uhuru wa kutembea – Ikiwa bei inaswihi

Inatoka Uk. 25

Mfumo wa usafirishaji Beitbridge

Kuna msururu wa magari unaopitia njia zisizo rasmi. Mahali fulani kama dakika 45 kutoka Musina, The Continent imezungumza na “mfanyabiashara” mmoja ambaye amekuwa akifanya kazi mpakani tangu 2018.

Anaitwa Mukoma Jimmy ambaye amekuwa akiendesha lori la tani 15 kutoka kwenye ukingo wa Mto Limpopo kutoka na kuingia Zimbabwe kila siku.

Jimmy ambaye anadai kuwa – kwa uzoefu wake, amekuwa na urafiki wa karibu na maafisa wa Uhamiaji, polisi, maafisa wa kodi, na wanjeshi pande zote mbili, hivyo kufanya kazi na maisha yake kuwa rahisi.

Anasema amekuwa akiaminiwa na watu wa pande zote mbili; Zimbabwe na Afrika Kusini na hiyo imemrahisishia biashara zake kuwa za uhakika.

Ukaribu wake na maafisa wote hao wa mipakani, kumemfanya kufanya kazi nzuri na kupata faida kubwa zaidi.

Jimmy, pamoja na wafanyabiashara wengine katika mtandao unaojulikana kama “usafirishaji wa Beitbridge,” hununua bidhaa kwa bei nafuu zaidi Afrika Kusini na kuzipeleka kwa wateja wa Zimbabwe.

Mfanyabiashara huyo hupokea ‘oda’ za vifurushi vya chakula, vifaa vidogo na vikubwa vya umeme, nguo, pombe, sigara, na hata vifaa vya kufuga nyuki.

Anashirikiana na vijana wachache wanaofanya kazi ngumu, mara nyingi katika joto kali, ambao hupakua bidhaa kutoka kwenye lori na kuzipakia kwenye mikokoteni inayovutwa kwa punda mtoni, ambayo hupitia msitu hadi kufikisha bidhaa hizo Zimbabwe.

“Vijana hawa wangekuwa nyumbani hawafanyi chochote, au mbaya zaidi, wakiingia matatani kama nisingewapa kazi, maona [unao-na]? Mimi ni mwajiri.”

Hawasafirishi watu, sigara haramu – wala

magari yaliyoibwa katika matukio ya kutisha ya utekaji nyara, jambo linalozidi kuwa tatizo.

Magari yaliyoibwa husafirishwa kwingine – katika maeneo kama shamba la Bi J.

Bi. J ambaye hataki kutambulika, anaendesha shamba la mifugo lenye mafanikio siyo mbali na mahali ambapo kikosi cha Jimmy hupakia na kupakua mizigo kwenye lori lake.

Misafara ya magari yaliyoibwa hukatiza shambani kwake kwa Jimmy, mara nyingi usiku, yakielekea kwa wanunuzi Zimbabwe na Msumbiji.

Ni operesheni ya hali ya juu: mitandao ya kihalifu ya wizi wa magari hutumia hata drones kuepuka kugundulika – kwa kugundua wako wapi ili kuwakwepa.

Kushindwa kuwakamata majambazi hao, ni kama Polisi na jeshi hawawezi kufanya lolote.

Mara kwa mara, gari lililoibwa Afrika Kusini hupatikana shambani kwake. Ndani ya magari hayo kuna dalili za safari zilizokatishwa kikatili.

Madoa ya damu huonekana kila kona ya magari hayo, hali inayoashiria kuwepo kwa tukio baya la kukatisha maisha ya dereva na pengine abiria waliokuwamo.

Ili kudhibiri ujambazi huo, utashi wa kisiasa au nguvu za ziada za Jeshi la Polisi zinahitajika zaidi, bila hivyo, kudhibiti ujambazi ni kazi hatari isiyomithirika.

* Makala haya yenye kubeba maudhui ya ‘Borderlands’ ni mfululizo mpya kwenye gazeti la The Continent, linaloangazia hali ya mipaka ya Afrika. Mfululizo huu umewezekana kwa msaada wa Umoja wa Afrika na GIZ. Pambazuko hushirikiana na gazeti hilo kusambaza habari kwa wanaofahamu Kiswahili.



Photo: Zinyange Aunty/The Continent

Habari



Kaimu Mkurugenzi wa TPA, Abed Gallus

TPA kuwapa afueni ya tozo manusura K'koo

Na Mwandishi WETU

FALSAFA kwamba “wakati wa majanga, ndipo rafiki wa kweli huonekana” – imedhihiri kuwemo ndani ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Bandari Tanzania (TPA).

Pamoja na kwamba TPA, inajukumu la kuku-sanya tozo kutoka kwa wafanyabiashara wanaotumia miundombinu yake, bado inawajali kipindi wanapopatwa na madhila.

Kufuatia ajali ya kuporomoka kwa jengo eneo la Kariakoo, Dar es Salaam na kusababisha madhara makubwa, ikiwamo vifo, TPA imeamua “kuwashika mkono” manusura, ikiwa ni ishara ya kuwajali na kuthamini mchango wa wafanyabiashara hao wa maendeleo ya taifa.

TPA imeamua kuwapunguzia gharama za uhifadhi mizigo (storage fee) manusura wote wa jengo la ghorofa liliporomoka katika maeneo

ya Soko Kariakoo, Novemba, 16, 2024.

Kaimu Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Abed Gallus, amesema kwamba TPA ina utaratibu wa kupunguzia gharama za uhifadhi wa mizigo kwa manusura wa majanga ambao ni wateja wa Bandari.

Amesema kwamba utaratibu wa kuwapa nafuu wadau waliopatwa na majanga pale wanapotoa taarifa ni wa kawaida na TPA imeshafanya hivyo mara kadhaa kwa utaratibu huu.

“Kuna janga na janga. Lipo janga mtu atandolewa na tozo ya asilimi 50; kuna majanga mengine, kulingana na ukubwa, mdau anaweza kuondolewa tozo kabisa,” amesema Gallus.

Amefafanua kwamba ili mfanyabiashara anufaike na heri hiyo kutoka TAP atatakiwa kutoa taarifa ya janga liliomkuta kwa wakala wake wa forodha na wakala atawasilisha taarifa hiyo kwenda kunakohusika kwa ajili ya hatua.

Gallus ameeleza kuwa kwa mantiki hiyo, wafanyabiashara waathirika wa janga la Kariakoo wanatakiwa kuwasiliana na mawakala wao wa TPA ili mchakato wa nafuu na heri hiyo uanze haraka.

“Kwa utaratibu wetu, tunahifadhi bure mzigo wa mfanyabiashara bandarini kwa siku tano tu. Baada ya hapo mfanyabiashara atatozwa kodi ya mzigo wake kulingana na siku mzigo huo utakapokaa bandarini,” amefafanua.

Pia amesema kuwa TPA inawapa pole inawapa pole wafanyabiashara waliokutwa na tukio hilo, wakiwa ndiyo wadau wakuu wa bandari hiyo.

Hadi jana taarifa zinaeleza kuwa kulikuwa na vifo 20 vilivyosababishwa na ajali hiyo, huku kukiwa na majeruhi wanaofika 90.

Rais Samia Suluhu Hassan alitembelea jengo lililoporomoka na kuelekeza kuwa majengo yote eneo la Kariakoo yakaguliwe upya na kwamba jengo litakalothibitika kuwa na hatari, libo-molewe.

Sababu ya kuanguka kwa jengo hilo bado haijafahamika, ambapo tayari Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kwa maagizo ya Rais Samia, ameunda tume maalum kwa ajili ya ukaguzi wa uimara wa majengo katika eneo hilo kitovu cha biashara na kodi kwa Tanzania. kitovu cha biashara na kodi kwa Tanzania.

Mjadala waibuka 'wanafunzi-wazazi' kurudi shuleni



Na Hellen NGOROMERA

YAWEZEKANA uamuzi wa serikali kuwarejesha shuleni wanafunzi wanaojifungua haukufanyiwa utafiti wa kina.

Sasa inaelezwa na wadau kuwa uamuzi huo wa serikali umechochea ongezeko la wasichana kupata mimba wakiwa shuleni.

Hatua hiyo ya serikali kuwarejesha shuleni wanafunzi wanaopata ujauzito inadaiwa kuchochea baadhi ya wasichana waliopo shuleni kujiingiza kwenye mapenzi wakitambua kwamba hata wakipata mimba, wataendelea na masomo baada ya kujifungua.

Rais Samia Suluhu Hassan ndiye aliyebariki wanafunzi hao kurejea masomoni akitofautiana na mtangulizi wake, John Pombe Magufuli aliyepinga mwanafunzi atakayepata ujauzito kurudi shuleni.

Magufuli alizungumza hayo katika moja hotuba zake alizozitoa mwaka 2017 na kuzitaka taasisi zinazotetea utaratibu wa wanafunzi waliopata mimba kurudi shuleni, kufungua “shule zao za wazazi” lakini siyo kuilazimisha serikali kuwapokea tena wanafunzi –wazazi hao.

Rais Magufuli alitoa agizo hilo siku chache

baada ya Taasisi ya HakiElimu kuitaka serikali kuharakisha kupitia na kupitisha miongozo ya watoto wa kike waliojifungua warejee shuleni na kuendelea na masomo.

Uamuzi huo wa kurejesha masomoni wanafunzi-wazazi, ulianza kutekelezwa na serikali ya awamu ya sita, umezua maswali mengi kutokana na athari ambazo zinaanza kuonekana.

Katika mkutano wa Bunge uliomalizika kari-buni, Mbunge wa Viti Maalumu, Fatma Toufiq (CCM), aliibua hoja hiyo kupitia swali alilolielekeza kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mbunge huyo alitaka idadi ya wanafunzi waliorudi shule baada ya kujifungua tangu serikali iwaruhusu kuendelea na masomo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Elimu, Omary Kipanga, alisema hadi kufikia Machi 2024, jumla ya wanafunzi waliojiunga tena na shule baada ya kukatiza masomo kutokana na ujauzito walikuwa 22,844.

Anasema kati yao waliorejea kwenye mfumo rasmi wa masomo ni 5,142 na 17,702 walirejea kupitia mfumo usio rasmi.

Katika jibu hilo, Naibu waziri alisema wanafunzi hao walirejeshwa shuleni kwa mujibu wa miongozi iliyomo katika Waraka wa Elimu Na. 2 wa Mwaka 2021 kuhusu urejeshwaji shuleni kwa wanafunzi waliokatiza masomo katika ngazi ya elimu ya msingi na sekondari, kwa sababu mbalimbali ikiwemo ujauzito.

Waraka huo unaelekeza kuwa wanafunzi waliokatiza masomo yao kutokana na ujauzito au uoto, wataruhusiwa kurudi shuleni ndani ya miaka miwili tangu walipokatika masomo yao.

Waraka pia unawataka wakuu wa shule na walimu wakuu wahakikishe mwanafunzi aliyekatiza masomo anarejea mwanzoni mwa mwaka wa masomo katika darasa alilokuwa anasoma.

Wabunge wanena

Lakini jibu hilo halikumtosheleza Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara (CCM) ambaye kupitia swali la nyongeza akiitaka serikali kutoa takwimu pia za wanafunzi walioolewa bada ya kupewa ujauzito.

Inaendelea Uk. 34



Habari

Mjadala waibuka ‘wanafunzi-wazazi’...

Inatoka Uk. 33

“Hiyo itatusaidia kujua ukubwa wa tatizo na kuwa siyo wanafunzi wote waliopewa mimba wamerejea shuleni,” alisema.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Elimu alisema; “tuna takwimu ambazo tunazichukua kila mwaka katika shule zetu zote. Kwa hiyo tuna takwimu za kila mwanafunzi, mahala alipo na amekatisha masomo kwa namna moja au nyingine.”

“Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa elimu kwa wanafunzi wa kike, serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaendelea kusimamia utekelezaji wa

Waraka tajwa ili kuhakikisha kuwa wanafunzi waliopata ujauzito wanarejea shuleni na kutimiza ndoto zao za kielimu,” aliongeza.

Akizungumza na Pambazuko kwa njia ya simu, Toufiq alisema idadi ya wanafunzi wanapata mimba wakiwa shuleni ni kubwa, hivyo serikali inatakiwa kuchukua hatua za haraka kudhibiti ongezeko hilo...”

“Baadhi yao wanapata mimba kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo umasikini, kwani wengi huishi katika mazingira duni, umbali wa shule pia huweka vishawishi kwao...”

“Kuna haja kwa serikali kujenga hosteli kwenye shule za kata ili kuwasaidia wanaoishi mbali na shule,” alisema mbunge huyo.

Aliongeza kuwa serikali inatakiwa kuweka programu maalumu ili kuwawezesha wanafunzi wa kike na wa kiume kuelimishwa athari za mimba za utotoni kwani wakati mwingine wanafunzi hao hupeana mimba wenyewe kwa wenyewe.

“Hata kwenye swali langu bungeni nilisema kwamba idadi yao inaongezeka tunatakiwa kupiga kelele ili idadi ya wanaopata mimba isizidi...”

“Wakati sisi tunakua tulikuwa tunawakimbia wanaume, lakini hali imebadilika hivi sasa...”

“Tukishirikiana kwa pamoja tutakomesha vitendo hivi. Malezi na makuzi katika familia liwe ni suala la kuangalia pia,” alisema Toufiq.

Mwanaharakati wa kutetea haki za binadamu, Dkt. Hellen Kijo Bisimba alisema kuhusu wanafunzi kurudishwa shuleni hilo halina mjadala, ni haki yao kupata elimu.

Dkt. Bisimba ambaye alikuwa akizungumza na Pambazuko alisema kinachotakiwa ni mfumo sahihi wa kuwarejesha wanafunzi hao shuleni.

“Kwanza wanafunzi hao ijulikane watawalea vipi watoto waliowazaa pindi watakaporudi shuleni. Isitokee kuwa wanapata unyanyapaa na kuwafanya washindwe kuendelea na masomo,” alisema Dkt. Bisimba.

Jambo jingine ni elimu ya afya ya uzazi. Hii haitolewi kwa watoto wanaofikia balehe, hivyo kujikuta wakipata mimba wakati mwingine bila kujua.

Kwa upande wake, Agatha Charles, ambaye ni mwalimu wa shule ya msingi, alisema kuna haja kwa serikali kutoa elimu ya kina kwa watoto hao kuhusu mimba za utotoni.

Alisema idadi ya watoto waliopata mimba na kurejea shuleni iliyoripotiwa ni kubwa, hivyo ikiwa watapatiwa elimu itawezesha kupunguza kama siyo kulimaliza tatizo.

Rachel Josephat ambaye ni mwalimu wa shule moja ya sekondari Dar es Salaam, alisema hatua ya serikali kuwarudisha shule inawapa mabawa anafunzi hao kufanya wanavyotaka.

“Hii haipo sawa kabisa tunakubaliana tu na serikali lakini watoto hawa wameota mbawa wanafanya wanavyotaka sasa kwa sababu wanajua watarudi shule wakitaka,” alisema Mwalimu Rachel.

Jamila Mohamed alisema serikali kuwaruhusu wanafunzi hao kurudi shule itawafanya wanafunzi wengi kutokuwa makini wanapokutana na vishawishi.

Alisema msichana anaweza kujikuta amejijingiza katika uhusiano wakati yupo shule matokeo yake akajikuta amepata ujauzito na kwa kuwa serikali imeruhusu kurejea kwao shuleni akaona ujauzito hauwezi kumfanya kukatishiwa masomo yake ikiwa atahitaji kurudi.



Unyanyapaa tishio kwa wenye kifafa

Na Arodia PETER

KIFAFU ni ugonjwa sugu unaotokana na mtu kupata mshituko katika ubongo na kusababisha degedege au kuanguka.

Hali hii hutofautiana kutoka mtu mmoja hadi mwingine kulingana na ukubwa wa mshituko.

Shirika la Afya Duniani (WHO), kifafa ni moja ya hali kongwe zaidi duniani inayotambulika, ikiwa na rekodi zilizoandikwa tangu miaka 4,000 kabla ya kuzaliwa Kristo.

Ugonjwa huu husababishwa na kuzalishwa kwa umeme mwingi kupita kiasi katika kundi la seli za ubongo.

Tafiti za kisayansi zinaeleza kuwa sehemu mbalimbali za ubongo zinaweza kuwa chanzo cha utoaji umeme huo wa mwili usiokuwa wa kawaida.

Mshituko hutofautiana kutoka muda mfupi zaidi au mshituko wa misuli hadi degedege kali ya muda mrefu.

Mshituko pia unaweza kutofautiana mzunguko kutoka chini ya mshituko mmoja kwa mwaka hadi mara kadhaa kwa siku.

Hata hivyo, mtu kupata degedege mara moja haimanishi kuwa ana kifafa, kwani asilimia 10 ya watu ulimwenguni wamewahi kupata degedege mara moja katika maisha yao.

Kama ilivyo kwa mataifa mengine, Tanzania pia ni miongoni mwa nchi zenye watu wanaouguwa ugonjwa huo wa kifafa.

Chama cha wazazi wa watoto wanaoishi na kifafa (Uwakita) pamoja na wadau wengine walikutana jijini Dar es Salaam hivi karibuni kuweka mkakati wa pamoja juu ya ugonjwa huo.

Katika mjadala huo mambo kadhaa yalijitokeza, lakini unyanyapaa ulielezwa kuwa ni hatari na kikwazo kwenye suala zima la matibabu ya watu wanaoishi na ukifafa.

Daktari bingwa wa afya na magonjwa ya akili wa Hospitali ya Taifa Muhimbili - Upanga Dar es Salaam, Nururi Kitomari anasema zaidi ya watu milioni 50 duniani wanaishi na hali ya ukifafa ambapo asilimia 80 wanaishi kwenye nchi zenye hali duni, nyingi zikiwa Afrika - Tanzania ikiwemo.

Watu milioni 10 wanaishi Afrika na hali ya uki-



Daktari Bingwa wa Magonjwa Afya ya Akili Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dkt. Kuganda Said akizungumza katika kongamano lililofanyika mwishoni mwa wiki kuhusu changamoto za watu wanaoishi na kifafa.

fafa.

Anasema kuna uwezekano idadi hiyo imeongezeka hivi sasa kwa sababu takwimu hizo ni za zamani kidogo.

Dkt. Kitomari anasema mwaka 2022, WHO iligundua kuwa watu 45,000 nchini Tanzania wanaishi na hali ya ukifafa. Na kwamba idadi hiyo ni kwa wale tu wenye usajili wa kutafuta matibabu hospitalini.

Lakini kuna kundi kubwa nje ya hao wanaoendelea kufichwa nyumbani na wengine kutibiwa kwa waganga wa kienyeji na maeneo mengine kama kuombewa makanisani na kadhalika.

“Unaweza kuona kuna namba kubwa ya hawa ambao hatuwajui. Yaani ni asilimia 3.7 tu ndio wapo kwenye matibabu, hivyo, bado tuna kazi kubwa ya kufanya ili watu zaidi ya asilimia 96 waingie kwenye mfumo.

“Ni vizuri jamii ifahamu kuwa magonjwa haya yanaongoza kwa kuleta ulemavu, kwa sababu wengi wanafungiwa ndani wanashindwa kujishughulisha na shughuli za kijamii na kuzalisha kipato kwa sababu ya unyanyapaa, dhana potofu na mazingira ambayo wanapitia kila siku,” anasema Dkt. Kitomari na kuingezea.

Anaongeza; “unyanyapaa ni moja ya kizuizi kikubwa cha shughuli zote za kumtibu mtu anayeishi na hali ya ukifafa...”

Inaendelea Uk. 36

 Habari

Unyanyapaa tishio...

Inatoka Uk. 35

“Mwingine anajinyanyapaa mwenyewe kwa sababu ya malezi na makuzi kwenye jamii yake inayomuo-na mgonjwa wa kifaa kuwa ni mtu mwenye ‘mapepo’, bahati mbaya, mkosi na majina mengine mabaya...”

Aidha, Mratibu wa Afya ya Akili Manispaa ya Kinondoni, Dkt. Mwendo Peter, anasema mapambano dhidi ya maradhi hayo yanakabiliwa na changamoto kubwa ya unyanyapaa kwa watu wanaougua ugonjwa huo, jambo ambalo anasema linahitaji kampeni kubwa ya utoaji elimu kwa jamii.

Anasema unyanyapaa huo mkubwa umechangiwa na masuala mtambuka zikiwamo mila, desturi na tamaduni tangu zamani ambapo familia zilizokuwa na mtu anayeishi na kifafa zilikuwa zinatengwa.

“Hili jambo lina historia kutoka kwa mababu zetu kwamba mtu hawezi kuoa kwenye familia ambayo ina watu au mtu anayeugua kifafa; vitu hivyo vimeendelea hadi sasa na hivyo kupoteza watu na wataalam wenye uwezo mzuri kutumikia jamii kama watu wengine,” anasema.

“Kutokana na unyanyapaa huo, baadhi ya wagonjwa wanaamua kujinyanyapaa wenyewe kwa kutokwenda hospitali na ndugu zao; mwingine anakuja kituo cha afya kwa kujificha ili watu wasimuone...”

“Mtu wa aina hii hawezi kusikiliza sawa sawa ushauri na maelekezo ya daktari au mshauri wa ustawi wa jamii kuhusiana na maradhi yake,” anasema.

Kutokana na hali hiyo, Dkt. Peter anasema mgonjwa wa namna hiyo hata akipewa dawa haiwezi kumsaidia kwani anaweza kufika nyumbani asizitumie kwa usahihi.

Aidha, daktari huyo anashauri watumishi wanaowahudumia wagonjwa wanaoishi na kifafa wapatiwe elimu ya ziada ili kuendana na mazingira ya sasa ya maendeleo ya teknolojia inayokwenda kwa kasi sana duniani.

Daktari huyo anasema asilimia kubwa ya watumishi katika vituo vya afya na hospitali wanatumia mbinu na elimu waliyoisoma darasani tu ambayo kwa sasa haitoshi. Anasema wanahitaji kuongezewa ujuzi wa mara kwa mara ili waweze kuendana na wakati.

“Utaalam wetu umepitwa na wakati, kile tulichojifunza darasani ni kilekile, hatuna cha ziada. Hivyo litakuwa jambo la msingi watalaam wetu waka-

ongezewa ujuzi kupitia mafunzo mbalimbali,” anasisitiza.

Kuhusu kupatikana dawa kwa watu wanaoishi na kifafa, Dkt. Peter anasema ni changamoto nyingine inayopaswa kuangaliwa kwa jicho la pekee.

Anatolea mfano wa Jiji la Dar es Salaam, kwamba dawa kwa ajili ya watu wenye kifafa zipo, lakini upatikanaji wake ni changamoto kwa sababu zinalipiwa.

“Kama mnavyojua asilimia kubwa ya watu wenye changamoto ya ugonjwa huo uwezo wao kiuchumi ni mdogo, hivyo hulazimika kutumia dawa zilizopo ambazo wakati mwingine daktari unatamani umwandikie mgonjwa dawa ambayo ingemsaidia zaidi, lakini wengi hawana uwezo wa kumudu gharama hizo,” anasema.

Mmoja wa wazazi mwenye mtoto anayeishi na changamoto ya kifafa, Jovina Josephati Hamis, anasema unyanyapaa unarudisha nyuma juhudi za matibabu ya ugonjwa huo nchini.

Anatolea mfano hospitali (jina tunalo) walioimpima mtoto wake na kugundua tatizo kwa mara ya kwanza. Anasema daktari katika hospitali hiyo alitaka kumsababishia hatari zaidi yeye (mama).

“Naweza kusema daktari wa hospitali ya ...(anaitaja) nilipofanya kipimo, daktari alikuja moja kwa moja ananiambia mtoto wangu ana ugonjwa wa kifafa...”

“Nilimwomba anielezee vizuri, lakini hakujali, aliniacha kwenye benchi la hospitali...”

“Nilipoteza mwelekeo na kusahau mlango wa kurudi nilipotoka. Alipaswa kuniandaa kisaikolojia, kunielimisha ili nipokee hayo majibu kwa utulivu...”

“Je, tunao madaktari wangapi wa aina hiyo? Je, wameandaliwaje kuelimisha wateja wao ambao ni wazazi au wagonjwa wenyewe?” anahoji.

Daktari bingwa wa magonjwa ya afya ya akili kutoka Hospitali ya Rufaa Amana Dar es Salaam, Dkt. Wanda Rwiza, anasema ili kupunguza unyanyapaa kwa watu wenye magonjwa ya kifafa, ni bora kutenganisha magonjwa hayo na yale ya akili.

Anasema mtu anayeishi na kifafa akienda hospitali akatibiwa eneo moja na wenye changamoto ya afya ya akili anapoteza matumaini.

“Jambo hili linawatisha, hivyo nashauri ugonjwa wa kifafa usichanganywe na wenye changamoto ya afya ya akili...”

“Hata watumishi wa afya kwa sababu ya kutokuwa na elimu ya kutosha wakiona mgonjwa wa kifafa, wanasema ni ‘mapepo,’ anasema Dkt. Rwiza.

Barua za Wasomaji

Wanaosajili simu mitaani chanzo cha wizi

Mhariri,

NIMESOMA kwa masikitiko sana habari kwenye gazeti hili la Pambazuko wiki iliyopita kuhusu jinsi Watanzania wanavyoibiwa mitandaoni.

Ukiisoma habari ile ni dhahiri kuwa vijana wanaopita mitaani wakijifanya kuwasaidia watu kusajili laini za simu au kuwawekea mitandao yenye kasi, ndiyo kwa kiasi kikubwa wanaotumika kufanya wizi huo.

Inashangaza kuwa kampuni za simu hazichukui hatua yoyote kuhusiana na vijana hawa ambao wanatembea wakiwa wamevaa mavazi yenye nembo za kampuni zao.

Na kama kampuni za simu zimeshindwa kuwachukulia hatua, basi serikali, ambayo ndiyo mlinzi mkuu wa wananchi, inapaswa kuchukua hatua sasa kuwapiga marufuku vijana hao hadi pale kampuni za simu zitakapoweka utaratibu salama wa kufanya shughuli hiyo.

Kama vijana hawa wasipodhibitiwa ni dhahiri kuwa wizi huu utaendelea.

**Yusuf Kutumbo,
Ilemela, Mwanza.**

Makondakta wachafu wadhibitiwe

Mhariri,

NAKERWA mno kwa namna makondakta wa daladala walivyo wachafu.

Kibaya zaidi uchafu huo wa nguo zao – uko kwenye sare za kazi ambazo nazo zimechanika na kuvaliwa juu ya nguo zingine.

Inapaswa makondakta hawa wafahamu kuwa wanafanya kazi ya kupakia abiria ambao wana hadhi tofauti, hivyo wanapaswa kuwa nadhifu.

Zaidi ya hayo, wakati mwingine nimepata kushuhudia namna wanavyobadilishana sare hizo jambo ambalo ni hatari kwa afya ya ngozi.

Ni vyema sasa makondakta na madereva wa daladala wakaheshimu kazi zao kwa kuzitunza sare ili ziwe nadhifu badala ya kusubiri kusimamiwa.

Vilevile mamlaka husika isimamie hili kwa kutoa adhabu kwa makosa ya uchafu kwenye sare za kazi.

**Diana Charles
Dar es Salaam.**

Ahadi hewa barabara ya Kimara-Bonyokwa hadi lini?

Mhariri,

NI miaka zaidi ya kumi sasa tangu tuahidiwe kuwekewa lami barabara ya Kimara-Bonyokwa yenye kilomita 1.2, lakini hakuna kinachofanyika.

Zaidi, kila uchaguzi unapokaribia wanaonekana watu wakichimba kwa greda na baada ya hapo hakuna kinachoendelea isipokuwa mateso kwa sisi watumiaji wa barabara hii.

Sasa tumechoshwa na ahadi hewa za viongozi, mfano juzi zilipoanza tu kampeni za uchaguzi wa serikali za mitaa, wakaanza kuchimba tena.

Na kipindi cha mvua hali huwa ni mbaya sana, sasa sijui hawa viongozi sijui wapo kwa ajili ya nani?

Inashangaza zaidi kuona pia kuwa kutokana na ubovu wake, wenye daladala wanatoza wananchi nauli ya shilingi 700 badala ya 400.

**Ally Hamisi,
Mkazi wa Bonyokwa,
Dar es Salaam.**

Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba; +255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz

NUKUU



Uchawa unaua sana ubunifu, kwa sababu hauhitaji kufikiri, kubuni wala kutenda – wewe ni kusifu tu na kujipendekeza. Isiyokuwa bahati, hasara yake haitazamwi kwa makini – Godbless Lema, kiongozi wa Chadema.



Mtanzania kesi ya ugaidi Kenya kuhukumiwa

Na Mwandishi WETU

KESI inayomkabili Mtanzania anayejitaja kuwa mganga wa kienyeji ambaye anatumia kwa ugaidi nchini Kenya, inakaribia kukamilika baada ya kusikilizwa kwa miaka mitatu.

Omar Ilole Shija, (32), mtoto wa askari mstaafu, ameshitakiwa kwa makosa zaidi ya 15 ya ugaidi na Serikali ya Kenya.

Alifikishwa mahakamani kwa mara nyingine wiki iliyopita kukamilisha ushahidi wake anaoutoa kwa kuzungumza mahakamani hapo.

Baada ya kukamilika kwa hatua hiyo, kinachofuata sasa ni pande zinazopingana katika kesi hiyo kuwasilisha ushahidi kwa njia ya maandishi katika kipindi cha wiki mbili.

Mtanzania huyo ameshitakiwa mbele ya hakimu mwandamizi Rita Orora katika mahakama ya Mombasa. Anatetewa na wakili Chacha Mwita.

Katika utetezi wake, Shija alieleza kuwa aliitwa nchini humo mwaka 2021 na shemeji yake ili kumhudumia mgonjwa aliyekuwa mahututi.

Lakini, alichodhani kuwa itakuwa ni safari salama ya kutoa huduma za tiba ya kienyeji, ikageuka kuwa madhila makubwa na jinamizi kwake.

Aliiambia mahakama kuwa alikamatwa na kabla hajajua nini kinatokea alijikuta akitupwa mahabusu katika Gereza la Shimo la Tewa mjini Mombasa akiwa mtuhumiwa wa ugaidi.

Tangu hapo, alieleza, maisha yake yakawa ni mahakamani ambako anakabiliwa na mashitaka kadhaa ya ugaidi.

Maisha ya Mtanzania huyo yalibadilika ghafla Novemba 19, 2021, alipokamatwa katika barabara ya Old Malindi mjini Mombasa, na kufikishwa kwenye kituo cha polisi.

Kwa mujibu wa ofisa kutoka taasisi ya kupambana na ugaidi nchini humo (ATPU), Geoffrey



Jengo kubwa la maduka la Westgate likiwaka moto kufuatia shambulio la kigaidi lililotokea Septemba 23, 2013 jijini Nairobi. (Picha na Maktaba)

Omete, Shija alikamatwa akituhumiwa kuwa mwanachama wa kundi la kigaidi la Al-Shabaab na pia kuingia Kenya bila ya kuwa na vibali.

“Uchunguzi wetu wa awali unatuaminisha kuwa Shija ni mwanachama wa kundi la kigaidi la Al-Shabaab, lenye matawi nchini Somalia, Kenya, Tanzania, Kongo, na Msumbiji. Inaaminika kuwa kundi hilo lina uhusiano na ISIS,” Omete aliiambia mahakama awali.

Ofisa huyo alituhumu kuwa Shija alikamatwa wakati akiwa njiani kwenda kujiunga na kundi hilo na kwamba hakuwa na nyaraka zozote zinazomtambulisha wala makazi nchini humo.

Ofisa huyo aliongeza kuwa Shija alikamatwa na maofisa wenzake waliomtuhumu kuwa mwanachama wa kundi hilo la kigaidi.

Awali Shija alishitakiwa kwa makosa mawili – kuwa mwanachama wa kundi la kigaidi na kuingia Kenya kinyume cha sheria.

Lakini baada ya uchunguzi wa kina uliofanywa, mashitaka yake yaliongezeka hadi 17 huku mengi yakihusiana na ugaidi kama vile kukutwa na vitu vinavyohusiana na ugaidi na kukusanya taarifa kinyume na kifungu cha 29 cha sheria ya kupambana na ugaidi nchini humo ya mwaka 2012.

Inaendelea Uk. 39



Mtanzania kesi...

Inatoka Uk. 38

Tangu afikishwe mahakamani hapo, Shija amesisitiza kuwa ahusiki na tuhuma hizo.

Katika ushahidi wake awali, uipande wa mashitaka uliieleza mahakama kuwa Shija alikutwa na kanda za picha jongefu na kanda za sauti, vikitajwa kama vifaa vyenye ujumbe unao-saidia shughuli za ugaidi.

Kanda hizo, zilizochezwa mahakamani hapo kama sehemu ya ushahidi, zilikua na sauti ya mwanaharakati wa Kiislamu, Shehe Aboud Rogo.

Ushahidi wingine uliowasilishwa na upande wa mashitaka mahakamani hapo ni pamoja na rekodi za simu ya mtuhumiwa, ikielezwa kuwa ilikuwa na taarifa za picha jongefu na sauti za mahubiri ya chuki.

Lakini katika utetezi wake, Shija anasisitiza kuwa yeye ni mganga wa kienyeji ambaye hafahamu kabisa masuala ya ugaidi.

Anasema aliingia nchini humo baada ya kuitwa na shemeji yake kwa ajili ya kutoa huduma ya tiba asilia.

Shemeji yake huyo, Peter Ndong'o, ambaye naye alikamatwa mwaka 2021, pamoja na Shija, naye alitoa ushahidi wake akimtetea shemeji yake.

"Nimewatibu watu wengi sana katika maeneo ya Kuria na Migori. Ndio maana (shemeji yangu) aliniita," Shija alieleza mahakama.

Anasema aliitwa kumapatia tiba bosi wa kaka wa shemeji yake na baada ya matibabu hayo kwenda vizuri alilipwa KSh10,000, sawa na TSh200,000, ambazo sehemu yake alizitumia kununua zawadi kwa ajili ya mke na watoto wake.

Anasema Novemba 19, 2021 aliamua kurejea nyumbani lakini wakati akisindikizwa na shemeji yake kuelekea kituo cha mabasi cha Mwembe Tayari, walizingirwa na watu wenye silaha katika barabara ya Old Malindi.

"Wakapiga kelele, 'Ni hawa hapa,'" alisema Shija, na kuongeza kuwa yeye, shemeji yake na dereva wa gari waliyokuwa wamepanda walizib-

wa usoni na vitambaa na kuchukuliwa kwenda kuhojiwa.

"Wakati wa mahojiano alikuwa wanasisitiza kuwa mimi ni Seif, mtuhumiwa wa ugaidi kutoka Somalia ambaye alikuwa anatafutwa. Nikawaeleza kuwa mie si Seif bali ni mganga wa jadi kutoka Tanzania ambaye sina uhusiano wowote na masula ya ugaidi. Lakini hawakunisikiliza," aliiambia mahakama.

Anasema yeye alihojiwa toauti na shemeji yake na dereva ambao baadaye waliachiwa.

Aliiambia mahakama kuwa simu yake ni aina ya Techno Spark 7, na si aina ya Techno KF6I ambayo waendesha mashitaka aliileta mahakamani kama ushahidi.

"Hiyo simu ya Techno KF6I si yangu. Sijawahi kutumia Telegram. Mimi ni mganga wa kienyeji tu. Sijui chochote kuhusiana na ugaidi. Mungu awasaheme maofisa walionitendea hivi, mimi nimeshawasaheme," alisisitiza.

Shija aliiambia mahakama kuwa hafahamu chochote kuhusiana na Aboud Rogo, ambaye video zake zilitolewa kwenye simu iliyoletwa mahakamani hapo ambayo si yake.

Ushahidi wake uliungwa mkono na Ndong'o, ambaye naye aliiambia mahakama kuwa mtu huyo ni mganga wa tiba asilia.


"Tunamfahamu kama mganga wa kienyeji kwa sababu ni shemeji yangu. Simu yake ni Techno Spark 7; sijawahi kumuona akiangalia video zilizoletwa mahakamani kwenye simu hiyo. Yeye ni Muislamu na mimi ni Msabato; tumekuwa tukiishi kwa upendo tangu amuone dada yetu," alisema huku akilia kwa uchungu.

Ndong'o aliiomba mahakama kurejea ushahidi uliotolewa na upande wa mashitaka na kumuachia Shija, ambaye anaamini alikamatwa na kushitakiwa kimakosa.

Upande wa utetezi pia uliwasilisha mahakamani hapo barua kutoka kwa mwenyekiti wa kijiji cha Mlimani huko Old Shinyanga, ambako Shija alizaliwa mwaka 1992.

Barua hiyo inathibitisha kuwa Shija ni mtanzania ambaye ni mganga wa tiba asilia.

"Ni mganga wa tiba asilia, na hicho ndicho alichokwenda kukifanya Kenya. Ni Mtanzania," anasema mwenyekiti huyo, Peter Hungwi, katika barua hiyo.



Chalamila mikononi mwa Kamishna wa Maadili

Na Mwandishi WETU

MALALAMIKO kuhusu Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, akituhumiwa kuondoa uzito haki ya kuishi kutokana kutokana na kauli zake zinazovunja Katiba, yamewasilishwa mezani kwa Kamishna wa Maadaili, kwenye Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Pambazuko limethibitisha kuwa malalamiko hayo yamewasilishwa na Wakiki Tito Magoti, mwanzoni mwa mwezi huu wa Novemba, akitaka hatua zichukuliwe dhidi ya kiongozi huyo ikiwa ni hatua ya kulinda maadili ya viongozi.

Mmoja wa wasaidizi wa Jaji Sivangilwa Mwangesi ambaye ndiye Kamishna wa Maadili, alilieleza Pambazuko kuwa ni kweli barua hiyo ya malalamiko imepokelewa katika ofisi yake mwanzoni mwa mwezi huu wa Novemba na tayari imeshaanza kufanyiwa kazi.

“Ni kweli tumepokea barua hiyo ya mwana nchi aliyetajwa kuwa ni Tito Magoti inayohusu malalamiko juu ya kauli za Chalamila na tayari tumeshaipeleka kwa wahuika ili ianze kufanyiwa kazi,” alisema msaidizi huyo wa kamishna ambaye hakupenda kutajwa jina lake gazetini.

Katika mazungumzo yake na Pambazuko msaidizi huyo wa kamishna alieleza kuwa barua hiyo ilishafika katika ofisi za Kamishna huyo, Jaji Sivangilwa Mwangesi na aliahidi kufuatilia ili kujua ni hatua gani zinazofuata.

Kauli ya Tito

Akizungumzia malalamiko hayo, Tito Magoti alisema aliyawasilisha kwa njia ya mtandao kupitia baruapepe ya Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Oktoba 30 na alituma kwa njia ya mkono siku hiyohiyo.

Alisema aliamua kumpeleka kwa Kamish-



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila

ta wa Maadili ya Viongozi wa Umma mjini Dodoma kwa kuwa ina mamlaka maalumu ya kuwashughulikia viongozi wanaokengeuka.

“Nimempeleka huko kwa sababu hii sekretarieti ina mamlaka maalumu, ni sawa na ambavyo mtu mwingine angekwenda mahakamani kwa ajili ya kushtaki kwa mujibu wa sheria ya madhara, au mwingine angetaka DPP apelekea kesi ya jinai mahakamani, lakini hizo njia nyingine siyo nyepesi.

“Sasa kama wakiona inafaa, sekretarieti itamuita, watamsikiliza lakini pia wakiona inafaa wataniita na mimi nitapeleka ushahidi wote nilio nao, kwa sababu kuna ushahidi wa kauli zake ambao unathibitisha jinai, kwa hiyo kama tume ikishahshauri afutwe kazi na mamlaka ya uteuzi ndipo wengine kwa mamlaka zao wanaweza wakaingia hapo,” alisema.

Malalamiko yaliyowasilishwa

Katika barua yake ya Oktoba 30, 2024 kwa Kamishna wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma iliyopo chini ya Ofisi ya Rais, Tito Magoti alimwadikia Kamishna akisema anawasilisha malalamiko yake kutokana na matamko ya Chalamila, ambayo yanakwenda kinyume cha sheria za nchi.

Inaendelea Uk. 41



Chalamila mikononi...

Inatoka Uk. 40

Alisema Ibara ya 132(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 na kifungu cha 19 (2)(b)(e) inayohusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma (sura 398 R.E 2020), anawasili-sha malalamiko ya kuwepo uvunjifu wa Kanuni za Maadili, kifungu cha 6 (1) (a), (b) & (c) uliofanywa na kiongozi wa umma, Albert Chalamila anayehudumu kama Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa sasa.

Katika lalamiko la kwanza linalohusu ukiukaji wa Katiba, alidai kuwa Chalamila amekuwa akirudia mara kwa mara maneno ambayo yanaonesha kutumia vibaya mamlaka yake hatua inayomfanya asisitahili kuendelea kuwa kiongozi wa umma.

“Oktoba 23, 2024 Chalamila alinukuliwa na baadhi ya vyombo vya habari akisema kuwa: Tulikuwa na changamoto ndogo sana ya baadhi ya watu kuiba transfoma... sasa Mhe Makamu wa Rais... anachokifanya anatumia transfoma..., anaiba ile kopa mule ndani, anachukua yule mafuta... wale tuliwakamata, tuliwaeleza wanywe yale mafuta mpaka watakapoyamaliza, ndio ikawa sababu ya kukomesha wizi wa transfoma hapa kwetu Dar es Salaam,” anaandika Magoti.

Alimweleza Kamishna huyo kuwa Chalamila alitoa kauli hiyo mbele ya Makamu wa Rais, Dkt. Philip Mpango, ambaye alikuwa akizindua mpango wa nishati joto jijini Dar es Salaam.

“Chalamila alikiri kuwa watu waliouhumiwa kuiba mafuta ya transfoma katika mfumo wa usambazaji umeme waliadhibiwa, akithibitisha kuwa walinyweshwa mafuta waliyokamatwa wakiwa nayo. Haujulikana kama kuna hatua zozote za kisheria zilichukuliwa baada ya hapo, hivyo kuacha sintofahamu kuhusu afya zao baada ya hatua hizo.

“Inaonekana kuna ushahidi unaotokana na kukiri kwake ambao unawagusa watu walio-guswa na vitendo hivyo visivyo vya kibinadamu na kwamba adhabu ya Chalamila kwa watuhumiwa wa wizi huo wa mafuta ya transfoma haipo kisheria. Chalamila siyo mwendesha mashtaka, wala siyo mahakama na hana mamlaka ya kiu-

chunguzi wala hajapewa mamlaka ya kimahakama iliyopo kwa mujibu wa sheria,” alieleza.


Alisema suala jingine ni Uvunjifu wa vifungu vya sheria (kifungu cha 6 (1) (a), (b) & (c) cha Kanuni za Maadili), ambapo Chalamila alikiri waziwazi, suala ambalo ni ukiukwaji mkubwa wa Kanuni za Maadili, zinazoweka viwango vya maadili kwa viongozi wa umma ‘kufanya kazi kwa uaminifu, huruma, busara, kujizuia, kiasi na kuzingatia viwango vya juu zaidi vya maadili kwa imani hiyo ya umma, imani katika uadilifu, usawa na kutopendelea kwa Serikali kunahifadhiwa na kuimarishwa.’

“Kwa mujibu wa Kanuni za Maadili, Chalamila anapaswa kuongozwa na misingi ya sheria na maslahi ya umma. Katika muktadha huu, kiten-do cha Chalamila kukiri uhalifu ni ukiukaji wa wazi wa Kanuni za Maadili zinazotumika kwa viongozi wa umma, kama ilivyoainishwa hapo juu. “Zaidi ya hayo, mwenendo wa Chalamila unaathiri misingi ya utawala wa sheria na utawala bora. Wanakiuka kanuni muhimu za haki ya asili, ikiwa ni pamoja na haki ya kusikilizwa, haki ya kudhaniwa kutokuwa na hatia na haki ya kuhukumiwa kwa haki, ambayo yote yamehaki-kishwa chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa tanzania-URT ya 1977,” alieleza kwenye malalamiko yake.

Maombi

Magoti alisema malalamiko haya yanatumika kama ombi rasmi kwa ofisi yako kwa: kumuita na kumhoji Chalamila kuhusu kukiri kwake kujihusisha na uhalifu; Kuishauri mamlaka ya uteuzi ya Chalamila, Rais wa URT, kutengua uteuzi wake wa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam; Baa-da ya kukamilisha hatua za kiutawala, apeleke shauri hilo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Chalamila anayeshitakiwa kwa jinai mbele ya mahakama; na kuchukua hatua nyingine yoyote ambayo ofisi yako itaona inafaa na inafaa.

“Kwa kuwa hili si tukio la kwanza kwa Chalamila kukaidi, najitahidi kuwasilisha maelezo mazito ya ziada aliyoyatoa wakati wa kusikilizwa kwa suala hili. Natumai ofisi yako nzuri itazingatia jambo hili mara moja kwa nia ya kuzuia kuongezeka zaidi kwa ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na Chalamila,” alisisitiza.



PSSSF yaanza kulipa mafao kwa kikokotoo bora

Na Mwandishi WETU

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), umetekeleza maagizo ya serikali kwa kuanza kulipa mafao ya wastaafu kwa kutumia utaratibu wa kikokotoo kilichoboreshwa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete amebainisha hayo wiki iliyopita jijini Dar es salaam, mbele ya wastaafu watarajiwa wanao-changia PSSSF wakati wa semina ya kuwajengea uwezo wa namna bora ya kuishi baada ya kustaafu.

“Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, ilisikia kilio cha wastaafu, na leo hii ninapenda kutangaza rasmi kwamba hadi kufikia jana (Novemba 19, 2024), jumla ya wastaafu 10,414 ambao wamestafu kuanzia Julai 2022 na kuanza kulipwa kwa kutumia kikokotoo kile kilicholeta taharuki wameshalipwa mapunjo na kazi bado inaendelea.”

Kikwete alisema jumla ya wastaafu wapya 2,479 ambao wamestafu kuanzia Julai 1, 2024, wameshalipwa mafao yao kwa kutumia kikokotoo kipya kilichoboreshwa na kazi bado inaendelea..

Aidha, serikali imeridhia maboresho yafuatayo yafanyike kuanzia Januari 2025, ambayo ni pamoja na wastaafu ambao wengi wamekuwa wakipokea kile kima cha chini cha kiasi cha shilingi 100,000, sasa kuanzia pensheni ya Januari 2025 pensheni yao ya mwezi itaongezeka kutoka shilingi 100,000 hadi shilingi 150,000.00.

Alieleza kwamba wastaafu ambao walikuwa wakipokea pensheni ambayo ni zaidi ya 150,000, na wao watapewa ongezeko la asilimia 2 kila mmoja.

Katika maboresho hayo, pia mstaafu yoyote



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Ridhiwani Kikwete akizungumza na waandishi wa habari. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Abdul-Razaq Badru. (Na Mpigapicha Wetu)

anayepokea pensheni katika Mfuko wa PSSSF akifariki, mfuko huo utatoa kiasi cha shilingi 500,000 kwaajili ya maziko (funeral grant), huku mstaafu yoyote akifariki wategemezi wake wanaotambulika kisheria ya Mfuko, watalipwa mkupuo wa miezi 36 wa pensheni ya mwezi ya mstaafu husika.

“Utaratibu huu ulishaanza tangu Julai 2022 lakini ulikuwa unatumika kwa wastaafu waliokuwa wanalipwa kwa kikokotoo kipya, lakini sasa utaratibu huu unafunguliwa kwa wastaafu wote hadi wale waliolipwa kwakutumia vikokotoo vya zamani vya kwenye mifuko iliyunganishwa.” Alifafanua Kikwete.

Kikwete aliwahakikishia wastaafu kuwa ustahamilivu wa Mfuko wa PSSSF umeendelea kuimarika kutoka asilimia 22 hadi kufikia asilimia 36.4 hivi sasa.

Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Abdul-Razaq Badru, alisema, tangu kuanzishwa kwa Mfuko wa PSSSF tayari umelipa jumla ya mafao yenye kiasi cha shilingi trilion 10.46 kwa wanufaika 310,458.

Katika dhana ya kuhakikisha wastaafu wanafurahia ustaafu wao bila changamoto ya uchumi, PSSSF imejipanga kuanzisha mafunzo maalum kwao katika maeneo ya uwekezaji kwenye viwanda vidogo na kati, uwekezaji katika masoko ya fedha, kilimo biashara na ujasiriamali.



Dawa za ARV

Siyo Ukimwi pekee, magonjwa mengine yanaua

Salim MOHAMMED, Tanga

KATIKA miaka ya hivi karibuni, Watanzania wengi, hasa vijana, wanatambua kuwa Ukimwi ndiyo gonjwa pekee la zinaa lenye kuogofya.

Hawa – wengi wakiwa vijana, hawana ufa-hamu mkubwa juu ya kuwepo kwa magonjwa mengine. Hii ni kwa sababu Ukimwi “umeimb-wa” mno – miaka nenda rudi.

Magonjwa ya zinaa yanatajwa, ikiwamo Ukimwi, yanatajwa na wataalamu wa afya kuwa hatari kwani yanaweza kusababisha vifo, hivyo ni vyema yote jamii kupata elimu kuyahusu ili kuyaepuka.

Elimu ni muhimu kwa jamii kuhusu magonjwa haya ya zinaa ili kuyaepuka. Vyema kila mtu akatambua namna magonjwa hayo yanavyoambukiza, dalili na tiba zake.

Shirika la Afya Duniani (WHO), linaeleza kuwa zaidi ya watu milioni moja duniani wanaambukizwa magonjwa ya zinaa kila siku.

Takwimu hizi zinatisha na sasa yapasa familia; wazazi na walezi, serikali, viongozi wa dini,

walimu, wanasiasa na mashirika yasiyokuwa ya serikali, kutoa elimu juu ya janga hilo ambalo linatajwa kuathiri uwezo wa kujamiiana, uzazi na hatari ya ugumba.

Magonjwa ya zinaa yanatajwa kuwa tishio na kuelezwa kuwa yako zaidi ya 30 ambapo huathiri wanawake kwa wanaume - kwa kuziba mirija ya uzazi, huku magonjwa kama kisonono yakiathiri njia ya kupitisha mbegu kwa mwanaume na uzalishaji na ubora wa mbegu.

Magonjwa ya zinaa yanaweza pia kuambukizwa kutoka kwa mama hadi kwa mtoto wakati wa ujauzito, kujifungua au kunyonyesha, na mara nyingi madaktari husisitiza wakati wa kliniki ya uzazi, mjamzito kuongozana na mwenza wake ili kupimwa afya mara kwa mara.

Utafiti wa Hali ya Ukimwi Tanzania (2022/2023) umeonyesha kiwango cha maambukizi ya Ukimwi kwa watu wazima umepungua kutoka asilimia 4.9 mwaka 2016 /2017 hadi asilimia 4.4 kwa mwaka 2022/2023.

Takwimu za shirika la umoja wa mataifa linaloshughulika na masuala ya Ukimwi (Un-aids) limesema kuwa asilimia 40 ya maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU) duniani yako kwa vijana kuanzia miaka 15 hadi 24.

Katika Tanzania, pamoja na kuwepo kwa taarifa za kupungua kwa maambukizi kwenye baadhi ya maeneo, bado serikali imeona vyema kuendelea “kupiga kelele” kuhusu magonjwa ya zinaa na sasa imeboresha mkakati maalum kupitia Wizara ya Afya ambao unaitwa; Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi, Magonjwa ya Ngo-no na Homa ya Ini (NASHCoP).

Takwimu za Wizara ya Afya za mwaka 2017 hadi 2019 zinaonyesha kuwa idadi ya watu waliopimwa na kubainika kuwa na ugonjwa wa kaswende pekee ilipanda kutoka watu 16,015 hadi 26,592 zaidi kwa wajawazito.

Watanzania wanapaswa kutambua kuwa woga wao juu ya kuambukizwa Ukimwi, uwe huohuo kwenye magonjwa mengine ya zinaa ikiwamo kisonono, kaswende, pangusa, gono, na hapo ndipo jamii itajiepusha na hatari ya vifo vinavyotokana na kujamiiana kusikokuwa sala-ma.

Mwandishi ni mchangiaji wa gazeti hili an-ayepatikana kupitia namba; 0655 902929

Maombi ya Rais Samia kwa matajiri G20



Rais Samia Suluhu Hassan

Inatoka Uk. 21

“Tunaamini dunia yenye haki, ustawi na endelevu itapatikana pale ambapo nchi zinazoen-delea kama yangu zitapata msaada, rasilimali na uwakilishi unaohitajika kuhamasisha maendeleo endelevu,” alisema Samia.

Alihoji iwapo dunia itabaki kama ilivyo, swali litakaloulizwa mwaka 2030, itakuwa wangapi walioachwa nyuma na dunia na siyo walioshindwa kufikia malengo ya SDGs.

Alisema pamoja na vikwazo vilivyopo, Tanzania imefanikiwa kutekeleza mageuzi ya kisera na kimfumo, sambamba na uwekezaji wa kimkakati kubadilisha mifumo ya kilimo na chakula.

Vilevile aliionba G20 kuanza uhamasishaji wa Haki ya Maendeleo (SDRs) kwa Taasisi za Fedha za Afrika kama vile Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

Pia aliziomba nchi hizo mahitaji ya mfumo wa haki zaidi wa uratibu katika mfumo wa kifedha wa kimataifa ulipo sasa.

Kadhalika alisema Tanzania inatoa mwito wa kuongeza mifumo ya msamaha wa madeni, misaada na mikopo ya masharti nafuu ambayo itajibu mahitaji ya nchi.

Aidha, alisema Tanzania inaunga mkono ushirikiano wa nguvu kama vile Muungano wa Kimataifa wa G20, dhidi ya njaa na umaskini ili kuhamasisha ubunifu na ukuaji unaoshirikisha watu wote.

“Mkutano huu unadhihirisha dhamira ya pamoja ya kutoacha dunia kama ilivyo, lazima tuongeze juhudi zetu, na kuhamasisha ahadi zetu za kujenga dunia yenye haki, ustawi na haki kwa wote.

Maazimio ya mkutano wa G20

Pamoja na mambo mengine, miongoni mwa maazimio yaliyofikiwa na nchi hizo ni pamoja kuunga mkono mipango ya kusitisha mapigano huko Gaza na Lebanon.


“Tunasisitiza haja ya haraka ya kupanua mtiririko wa misaada ya kibinadamu na kuimarisha ulinzi wa raia na kutaka kuondolewa kwa vikwazo vyote vya utoaji wa misaada ya kibinadamu kwa kiwango kikubwa,” inasema sehemu ya tamko la maazimio lililotolewa baada ya mkutano huo.

Vita vya Israel dhidi ya Gaza hadi sasa vi-meua zaidi ya watu 43,900 na kujeruhi wengine 104,000. Tel Aviv pia inakabiliwa na kesi ya mauaji ya halaiki katika Mahakama ya Kimataifa ya Haki kwa hatua zake huko Gaza.

Tanzania ilipata mwaliko huku Rais Samia akiwa mkuu wa nchi wa kwanza kushiriki mkutano wa nchi hizo za G20 zinazochangia asilimia 85 ya pato la jumla la dunia na asilimia 75 ya biashara ya kimataifa.

Kabla ya Rais Samia, kiongozi wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa na wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete waliwahi kushiriki mikutano ya aina hiyo wakati umoja huo ukiitwa G8, kabla ya mabadiliko ya mwaka 2008.

G20 inajumuisha nchi za Argentina, Australia, Brazil, Canada, China, Ufaransa, Ujerumani, India, Indonesia, Italia, Japani, Jamhuri ya Korea, Mexico, Urusi, Saudi Arabia, Afrika Kusini, Uturuki, Uingereza na Marekani, kadhalika mashirika mawili ya kikanda, Umoja wa Ulaya na Umoja wa Afrika.



Na Hellen
NGOROMERA



Uhusiano



Mlee mume kama unavyolea watoto

MATUMAINI yangu ni kwamba mzima wa afya msomaji wangu wa safu hii ya uhusiano.

Wiki iliyopita nilizungumza namna siri za ndani zisivofaa kutolewa kwa marafiki.

Wiki hii nitazungumza wajibu wa mwanamke kwa mumewe.

Nilielea kwamba mwanaume ni kiumbe anayetakiwa kutunzwa na mkewe kwa hali zote katika kipindi chote cha maisha yao.

Mwanamke anapaswa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha anamshauri mumewe masuala ya kimaendeleo ili kuiwezesha familia yao kufanikiwa.

Wajibu wa mwanamke kwa mumewe uendane sambamba na kuhudumia familia kwa ujumla kwa kuhakikisha anawalea watoto wake ipasavyo kama vile kuwapatia mahitaji yote muhimu ya malezi bora, afya, elimu na mengine.

Kama ni mama wa nyumbani, mwanamke anapaswa kuilea vyema familia yake, huku akihakikisha anampatia mumewe ushauri mzuri wa kusogeza mbele maisha yao, lakini pia kujikita katika shughuli mbalimbali za uzaishaji mali kama biashara ndogo ndogo ambazo zitamwingizia kipato.

Kama ni mfanyakazi, anapaswa kuhakikisha majukumu yake ya kikazi hayaharibu ratiba zake za nyumbani kama mama.

Kwa ufupi, mke ndani ya nyumba anapaswa kumlea mumewe kama vile ambavyo anawalea watoto wake.

Wanawake wengi wanaofanya kazi maofisini, wamekuwa wakishindwa kutimiza majukumu yao kama wake kwa waume zao na familia, kwa kisingizio cha kutingwa na kazi nyingi, hali ambayo inafifisha ndoa zao.

Mwanamke anatakiwa kuhakikisha anakuwa msimamizi mkuu wa familia kwa kupanga majukumu vyema kwa mustak-

abali wa familia hiyo.

Anatakiwa kumshauri mumewe namna ya kutunza pesa na kuweka mipango thabiti ili waweze kujenga nyumba, kuweka miradi mbalimbali ya familia na vingine vya maendeleo.

Wanawake wengi wamekuwa na kasumba ya kuona kwamba shughuli pekee ambayo wanaweza kuifanya kwa familia ni kubeba mimba na kupata watoto, kufanya shughuli za ufuaji, upishi na nyingine ndogo ndogo na kusahau kwamba wamebeba majukumu makuu katika familia zao.

Kwa wale wenye tabia hizo waziache na kubadilika na kuwa bega kwa bega na waume zao katika kuhakikisha familia zao zinaishi misha bora.

Ni wakati wa mwanamke kusimama imara na kuhakikisha wanatambua wajibu wao na kuutenda kwa vitendo.

Tukutane wiki ijayo.

**Kwa maoni
len2ngoro-
com**

**na ushauri: hel-
mera@gmail.
Au simu:
0715 88
67 49.**



Mitindo & Urembo

Na Agatha Charles

Nguo za kupaki kwa ajili ya mapumziko

KWA sasa tuko katika kipindi cha maandalizi kuelekea mapumziko ya mwisho wa mwaka.

Maandalizi haya hayapaswi kuwa na chembe ya msongo wa mawazo.

Watu wanaojua mitindo na staili wanafahamu kitu cha kuweka wakati wa kupaki vitu vya kwenda mapumziko.

Tisheti nyeupe

Mwanamke unaweza kupaki tisheti nyeupe na kaptula ya pinki, ambavyo unaweza kuvaa utakapokuwa mapumzikoni.

Kofia

Kofia ni kitu kizuri kukiongeza katika mpangilio wako wa mavazi ya kwenda mapumzikoni ili kupunguza ukali wa jua. Kofia unaweza kuvaa hata ukiwa safarini.

Weka sketi fupi

Katika mpangilio wa nguo zako, weka sketi fupi uvae na shati unaloweza kustaili na tai ndogo kunogesha.

Jinzi ya bluu

Jinsi ya bluu na tisheti nyeupe vinakwenda sambamba. Paki suruali yako hiyo ukiongeza na tisheti pana, crop top ama top ndogo ya kubana.

Makobazi

Ni moja ya kiatu ambacho ni chaguo. Huko unakwenda kupumzika, viatu vyenye soli fupi ndiyo chaguo sahihi na hasa makobazi.

Shati la lineni

Shati la lineni lina hewa na nafasi ya kukufanya ujiachie. Ni chaguo bora pia.

Vazi la kuogelea

Panga nguo hata moja ya kuogelea ili uweze kutumia wakati wa mapumziko kupoza mwili wako.



Unavyoweza kuhifadhi hereni kwenye vifungo

WENGI wanasahau kununua vitu vya kuhifadhi hereni na kufanya zipotee zote ama moja.

Hapa nimekuweka njia mojawapo ya kuhifadhi hereni zako haswa wakati wa kusafiri.

Chukua nguo ambayo huitumii, toa vifungo vyake kisha weka hereni zako kwa kuzipachika kwenye hivyo vitundu.

Hii itasaidia kuhifadhi vyema na kuziweka pamoja hereni zako.

Kwa maoni na ushauri: piga simu 0656531217



Afcon



Afcon na usemi wa 'bure ni malio'

Na John MARWA

WASWAHILI wana msemu wao kuwa; 'bure ni malio, pasipo na sikio.'

Maana ya msemu huu ni mtu anapopatwa na madhila, basi wa kuyatatua ni yeye mwenyewe. Asitegemee mwingine.

Kauli hiyo inapewa ithibati na Timu ya Taifa ya Tanzania - 'Taifa Stars kwa kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika; Afcon 2025 baada ya kuwafunga Guinea bao 1-0, katika mchezo wa mwisho wa kundi H, kuwania kufuzu fainali hizo.

Ikumbukwe kuwa Tanzania ni mwandaaji mwambata wa Afcon 2027 yaani 'Pamoja Afcon' baada ya michuano inayofuata kukamilika nchini Morocco mwakani.

Washirika wengine wa maandalizi ya Afcon 2027 ni Kenya na Uganda ambao pia walikuwa viwanjani kuisaka heshima ya Afrika Mashariki na kuchochea kuni kwenye chungu cha maandalizi ya uenyeji wao ndani ya uwanja na nje ya uwanja.

Ni wazi maandalizi yanaenda vizuri nje ya uwanja ndio maana Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) limewapa kipimo cha uenyeji wa Fainali za Mataifa Afrika kwa wachezaji wanaocheza ligi za ndani (CHAN -2025).

Katika kuchochea maandalizi ya uenyeji wao, Tanzania na Uganda wameweka muhuri wa moto kwa kuibeba bendera ya Afrika Mashariki kwenda katika fainali zilizo mbele yao kabla ya kuyaalika mataifa mengine kwenye ukanda wa maziwa makuu.

Yawezekana kenya walisahau kuwa asiye bahati habahatishi, safari imefika mwisho.

Wakati Uganda wakifuzu mara ya nane na Tanzania mara ya nne, Afrika mashariki imefurahi.

Somo kubwa ni kwa Tanzania jinsi ilivyofuzu katika kundi lililokuwa na timu ambazo ni ngumu na shidani na zenye mafanikio makubwa zaidi kwenye mashindano hayo.

Congo DR ni mabingwa mara mbili wa mashindano hayo na Guinea ni washiriki zaidi ya mara 15 katika fainali hizo, lakini Tanzania bahati imeiangukia kwa kuwekeza na kuipambania bahati yao kutokana na ubora wa vijana wake.

Habari kubwa siyo Tanzania kufuzu, lakini ni kwa mara ya kwanza Tanzania inafuzu kwa pointi nyingi zaidi wakiwa na pointi 10 na wastani chanya wa mabao ya kufunga na kufungwa chini ya benchi la ufundi linaloongozwa na wazawa.

Uganda kufuzu kwao inaweza isiwe habari Afrika labda kwa wageni. Kenya kushindwa kwao siyo mwisho wa mapambano ni wazi matatizo yao wanayajua hivyo ni muda wa kuyatatua wenyewe bila kumtegemea mtu.

Ni wakati wa kutumia CHAN na Ligi yao kutatatua kwa haraka kabla ya 2027 ili 'Pamoja Afcon' isijekuwa inakaribisha wageni kuja kuaimbisha sebuleni, hai-tapendeza.

Tanzania na Uganda ni wakati wa kuhakikisha wanajiandaa vyema kwenda kupambana Morocco ili utamu uendelee.



Harmonize ampiga kijembe Diamond

Na Mwandishi WETU

NYOTA wa Bongo Fleva anay-etamba kwa sasa katika tasnia hiyo, Rajab Abdul Kahali maarufu kama Harmonize, amempiga kijembe msanii Diamond Platinumz kuwa huwezi kushinda tuzo za Grammy kwa wimbo wa kuwasalimia watu.

Harmonize alisema hayo jana wakati wa uzinduzi wa video yake mpya ya 'You better go' na kuelezea mpango wake wa kushinda tuzo za Grammy mwaka 2025/26.

"Huwezi kushinda Grammy kwa kuwasalimia watu, kwenye wimbo wako kwa kigezo cha umaarufu wako, Mimi nimeji-panga kushinda kwa ngoma kali na yenye ujumbe," alisema.

Maneno hayo ya Harmonize yalikuwa ni kijembe kwa bosi wake wa zamani Diamond aliye-wania tuzo hiyo kwa Ngoma yake ya 'Komasava'.

"Mimi ndio nitakuwa msanii pekee nitakayeshinda tuzo za Grammy mwaka 2025- 2026, kwani tuzo hizo hawaangalii umaarufu bali kazi zako, tufanye kazi. Umaarufu utakuja wenyewe kwa kufanya kazi nzuri".



Dhamana ya Diddy yagonga mwamba tena

Na Mwandishi WETU

MFANYABIASHARA na Msanii wa Rap Sean Combs maarufu kama "Diddy" amejitokeza tena mahakamani New York Ijumaa akiendelea kupigania kupewa dhamana katika kesi yake ya makosa ya jinai ya utapeli na usafirishaji haramu wa binadamu.

Mwakili wake walipendekeza aachiwe kwa masharti makali, ikiwa ni pamoja na kifungo cha nyumbani kwenye nyumba ya vyumba vitatu huku akilindwa saa 24 na walinzi wa usalama.

Hata hivyo, waendesha mashata walidai Diddy hawezi kua-minika kufuata masharti ya mahakama.

Waendesha mashtaka walisisitiza kuwa kesi hiyo ni kuhusu "ukatili," huku wakipinga usalama wake binafsi uliopendekezwa.





Mpaka waseme Ballon d'Or wameipataje?

Manchester, ENGLAND

Nini kimetokea? Nini kimewakutaka maana wanadharirishwa vibaya mno. Ni kama klabu zingine zimeamua ubaya ubwela kwa Pep Guardiola na jeshi lake la Manchester City katika michezo mitano mtawalia amepokea vipigo vikali.

Labda haijawahi kutokea kwa Bingwa Mtezi kupoteza michezo mitano mfululizo katika historia ya soka hasa kwa miaka ya hivi karibuni na kwa aina ya kikosi kama cha City ni dhahama nzito kwao.

City wamekuwa katika kiwango kibovu katika michezo mitano sasa ambapo walianza kupoteza kwa Tottenham Oktoba 30 katika mchezo wa EFL Cup kwa mabao 2-1, Novemba 2 wakupoteza nyumbani kwa Bournemouth mabao 2-1.

Novemba 5, wakupokea kichapo kizito kutoka kwa Sporting CP ya Ureno kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya cha mabao 4-1, wakiwa bado hawaelewi Novemba 9 Brighton wakapita nao kwa mabao 2-1 na juzi Tottenham wakatonesha kidonda kwa kuwakanda mabao 0-4 nyumbani Etihad.

Kabla ya kipigo cha mwisho Maboss wa Manchester City wamemuongeza kandarasi ya kusalia klabuni hapo Mhispania Pep Guardiola ambaye ameipatia timu hiyo mafanikio makubwa katika muda ambao amekupo klabuni hapo.

Swali ni je, shida wanayopitia ni kukosekana kwa mshindiwa Ballon d'Or Rodrigo Hernández Cascante 'Rodri' ambaye amekosekana katika michezo 12 kwa kuuguza jeraha la goti. Ama ni mzimu wa sokabaada ya kuchukua ubingwa wa EPL misimu mitatu mtawalia?

Ni timu iliyopoteza shauku ya mapambano ya soka na kuwa wazi kila eneo la uwanja jambo linalopelekea wapinzani kutoa adhabu kali, ukiwatazama wachezaji wa City ni kama hawakufanya maandalizi ya msimu kwa namna walivyo dhaifu katika utimamu wa mwili.

Kituo kinachofuata kwa Guardiola ni Anfield Decemba Mosi, kwenda kujiuliza kwa vijana wa Arne Slot ambao wako moto sana msimu huu. City watainua vichwa vyao na kuhesabika ama mwaka wa mateso utaendelea.

MICHEZO

Jumatatu, Novemba 25-Desemba 1, 2024



Wanaume wa Tanzania kazini CAF



Na John MARWA

Hii ni wiki ya kazi wiki ya wanaume kurejea katika anga ambazo wamekuwa gumzo miaka ya hivi karibuni katika soka la Afrika.

Wanarejea kwenye mapambano ya kusaka riziki yao katika ulimwengu wa kabumbu nje ya mipaka ya Tanzania.

Ni wiki ambayo wakongwe Kariakoo wakiongozana kusaka heshima mpya ama kuindeleza katika Ligi ya Mabingwa Barani Afrika (CAF CL) na Kombe la Shirikisho (CAF CC).

Hapa Yanga SC katika Ligi ya Mabingwa hatua ya makundi wakiwa kundi A, lenye miamba kama TP Mazembe (Congo DR), Al Hilal (Sudan) na Mc Alger (Algeria) ambapo kesho wa-

kianza kampeni dhidi ya Al Hilal, katika Dimba la Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Yanga watashuka dimbani kuwaalika Al Hilal wakiwa na kumbukumbu ya kuishia robo fainali msimu uliopita wakikwaa kisiki mbele ya Mamelod Sundowns ya Afrika Kusini.

Vijana wa Sead Ramovic wanaingia kwenye mchezo huo wakiwa na kumbukumbu ya kupoteza michezo miwili mtawalia ya ligi.

Yanga licha ya vipigo walivyovipata kutoka kwa Azam FC na Tabora United, wanachagizwa na ujio wa kocha mpya baada ya Miguel Angel Gamond kuonyeshwa mlango wa kutokea siku chache zilizopita.

Ni mchezo wa kusaka furaha kwa Watanzania dhidi ya mpinzani mgumu ambaye aliwaondosha kwenye mashidano hayo misimu mitatu nyuma kwenye hatua za mtoano.

Wakati huohuo, Simba ikiwa katika ujenzi mpya ya dunia yake katika soka, itashuka katika uga wa Benjamin Mkapa Jumatano hii kuwaalika Bravos do Maquis ya Angola katika mchezo wa kwanza wa hatua ya makundi Kombe la Shirikisho mtanange wa kundi A.

Katika kundi hilo, Simba yuko na Bravos ya Angola, CS Sfaxien ya Tunisia na Constantine ya Algeria.

Simba wanaingia kwenye mchezo huo wakiwa katika kiwango bora cha kushinda mechi zao msimu huu wakiwa vinara wa ligi.

Kila la heri kwa wakongwe hawa wa soka la Tanzania na miamba ya soka la Afrika Mashariki na kati katika harakati za kuisaka heshima mpya ama kuindeleza katika ramani ya soka Afrika.

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko - kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

